epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumanne Oktoba 8, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581823
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA WA 22

## TEN HAG ALIA UKAME WA MABAO MANCHESTER UTD

ERIK ten Hag amesema Manchester United lazima "iongeze nguvu" na kufunga mabao zaidi baada ya kupata sare tasa dhidi ya Aston Villa na kuendeleza...

# Jacob atoka kwa dhamana

• **Kuwalipia** mahabusu 10 faini... *Endelea ukurasa 2*



Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Pwani, Boniphace Jacob (katikati), akifurahia pamoja mawakili wake, Dickson Matata (kushoto) na Peter Kibatala, baada ya kupata dhamana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Mpina amtwisha Nchimbi mzigo kero wakulima, wafugaji

UKURASA 3

UKURASA WA 4

**Rais** Mwinyi aagiza taasisi kushughulikia kero za wazee

UKURASA WA 19

**DRC** yazindua chanjo ya M-pox



UKURASA WA 19

**Mahakama** Kuu Kenya yakataa ombi la kusitisha kesi ya kumfukuza Naibu Rais



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Plasduce Mbossa, akiwahudumia wateja wa mamlaka hiyo katika maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja, ambayo kaulimbiu yao ni 'Beyond and Above' na kuwashukuru kwa kuendelea kuchagua bandari za Tanzania kama njia kuu ya kusafirisha shehena. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

BINTI WA DOVYA

## Afande ashindwa kufika kortini

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA, YANGA SC MTEGONI CAF** UK.24 **KATUNI** UK.6

# Afande kesi ya binti wa Dovya, ashindwa kufika mahakamani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

HATIMA ya mshtakiwa wa kesi ya kuwatuma vijana kumbaka na kumwingilia kinyume na maumbile binti mkazi wa Yombo Dovya Dar es Saalam, Fatma Kigondo maarufu kama 'Afande' kuendelea kubaki mtaani kujulikana wiki ijayo.

Wakili wa upande wa mlalamikaji, Peter Madeleka, aliiomba Mahakama ya Wilaya Dodoma kutoa amri ya kumkamata na kumweka rumande mshtakiwa huyo kwa ajili ya usalama wake kama ilivyofanya kwa washtakiwa wengine.

Fatma, anakabiliwa na shtaka la kubaka kwa kundi kinyume na kifungu cha sheria namba 131 A, kifungu kidogo cha pili ambacho kinasema anayewasaidia wahalifu kutenda kosa la ubakaji na yeye anahusika kwenye ubakaji wa kundi.

Kesi hiyo ambayo ilipangwa kusikiliza jana, iliahirishwa hadi Oktoba 15, mwaka huu, baada ya mshtakiwa kutofika mahakamani kwa madai kuwa ni mgonjwa.

Wakili, Madeleka akiwasilisha hoja zake mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi wa mahakama hiyo, Nyambuli Tungaraja, aliiomba mahakama kutoa amri ya kukamatwa kwa Fatma na kumweka rumande katika Gereza la Isanga jijini hapa.

Wakili, Madeleka alidai mahakamani hapo kuwa kutoa amri hiyo ili mshatakiwa huyo akamatwe mara moja na kunyimwa dhamana kama ilivyokuwa kwa washtakiwa wengine.

"Mheshimiwa hakimu tunaomba mahakama yako tukufu itoe amri ya mshtakiwa kukamatwa na kuwekwa rumande na kuondolewa dhamana kwa sababu ya usalama wake kama ambavyo mahakama imekuwa ikitoa amri hizi kwa washtakiwa wengine.

"Lakini pia kutokana na mshtakiwa leo (jana) kutofika mahakamani hapa amevunja amri ya mahakama ambayo inamtaka kufika kila tarehe ya shauri lake, hivyo tunaomba mahakama itoe adhabu kali mara moja kwa mshtakiwa kuvunja amri ya mahakama ya kumtaka kufika kila shauri linapoendeshwa kwani kukosekana kwake hapa leo kesi hii haiwezi kuendelea," alisema Madeleka.

Wakali wa mlalamikiwa, Sedrick Mbunda, awali alieleza mahakama hiyo kuwa mteja wake hajafika mahakamani kutokana na ugonjwa na kuiomba mahakama impangie siku nyingine ya kusikilizwa shauri hilo.

Hoja hiyo ilipingwa na wakili Madeleka ambaye alihoji kama mshtakiwa huyo ni mgonjwa kwanini wakili huyo hajaleta ushahidi wa daktari mbele ya mahakama hiyo.

"Kama anaumwa lazima wangeleta ushahidi wa daktari kama ambavyo wanatakiwa kufanya kwa mujibu wa sheria, lakini hii kusema tu mtu anaumwa sio kazi ya mahakama kubaini kama mtu anaumwa kweli au haumwi, walipaswa kuleta ushahidi wa kimatibabu hapa sio kuzungumza tu," alisema Wakili Madeleka.

Hakimu Tungaraja, aliahirisha shauri hilo hadi Oktoba 15, hoja hizo zitakapotolewa uamuzi.

Septemba 5, mwaka huu, Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Dodoma iliahirisha shauri lililofunguliwa na Wakili Paul Kisabo dhidi ya Afande Fatma Kigondo anayetuhumiwa kuwatuma vijana kumbaka kwa kundi na kumwingilia kinyume na maumbile binti mkazi wa Yombo Dovya, jijini Dar es Salaam.

Kuahirishwa kwa shauri hilo kulitokana na hakimu aliyekuwa anasikiliza shauri hilo kuhamishwa kituo cha kazi huku shauri hilo likiwa halijapangiwa hakimu mwingine.




Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Prof. Elifas Bisanda (wa tatu kulia), akizungumza na wanafunzi 12 pamoja viongozi 3 wa chuo hicho, wanaokwenda Ujerumani kwenye mafunzo maalumu ya elimu jumuishi katika hafla iliyofanyika chuoni hapo jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa OUT Mara, Dk. Asha Katamba. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Jacob apata dhamana atoa mambo matano mazito

**Na Waandishi Wetu**

ALIYEKUWA Meya wa Kinondoni na Ubungo, Boniface Jacob, maarufu kwa jina la 'Boni Yai' ametaja mambo matano aliyojifunza akiwa mahabusu atakayokwenda kuyasimamia baada ya kutangazwa mshindi wa nafasi ya Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Pwani.

Akizungumza jana katika viunga vya Mahakama ya Kisutu baada ya kupata dhamana hiyo, alisema kukaa kwake gerezani kumemsaidia kuifahamu nchi, kwa kuwa alikutana na wafungwa waliomweleza matatizo yao.

Alisisitiza uzoefu alioupata anataka kuutumia katika kuendeleza mapambano yake kudai haki kwa Watanzania, hasa waliokosa fursa za kisheria.

Alisema kutokana na funzo alililopata atawalipia wafungwa 10 faini wanazodaiwa katika Gereza la Segerea, huku mmoja akiwa tayari amelipiwa faini na wengine tisa wakikamilishiwa leo ili wawe huru.

Pia, aliahidi kuwatafutia mawakili na kulipa gharama, wafungwa 20 wa makosa mbalimbali, mengine yakiwa hayana dhamana katika gereza hilo.

Alisema ameamua kufanya hivyo baada ya kuwasikiliza na kubaini wanahitaji msaada wa mawakili wa jopo kama alilonalo, alidai tayari amechukua orodha yao na ataikabidhi kwa mawakili ili waanze kushughulikia.

Akizungumzia hali ya watu waliopotea au kutekwa, Jacob alisema kero hiyo lazima iishe, na kama itaendelea, yeye atakuwa mstari wa mbele kuendelea kupambana, hata kama atakwenda jela mara kwa mara.

**USHINDI**

Pamoja na changamoto za kuwa gerezani, Jacob aliibuka mshindi wa nafasi ya Mwenyekiti wa Kanda ya Pwani ya CHADEMA katika uchaguzi uliofanyika Oktoba 5.

Katika uchaguzi huo uliofanyika Kibaha, mkoani Pwani, alipata kura 60 sawa na asilimia 77, akimshinda mpinzani wake Gervas Lyenda, aliyepata kura 17. Akiwa mwenye furaha kwa ushindi huo, Jacob alisema wanachama wa CHADEMA wamempa deni la utumishi kwa miaka mitano ijayo, atahakikisha Kanda ya Pwani inakuwa yenye heshima, haki, na usawa.

Alisema atahakikisha kuwapo kwa usawa wa kisiasa na haki za jinai, huku akikazia umuhimu wa kuunganisha vijana waliosoma sheria na hawana ajira kunufaika na eneo la haki jinai ambao litakusanya watu wa kada hiyo ili kuwasaidia wananchi kupata haki zao.

**MNYIKA**

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alipongeza uamuzi wa kumpa Boniface dhamana kwa kuwa hakukuwa na haja ya msingi ya kumnyima haki hiyo.

Aidha, alisema kutoka kwake kwa dhamana hakumfanyi kuwa huru kwa kuwa bado ana kesi inayoendelea na kuiomba Jamhuri ipeleke hati ya kutokuendelea na kesi hiyo kwa kuwa anaona haina mashiko.

**MAHAKAMANI**

Jana Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, ilimpa dhamana Boniface baada ya kusota rumande kwa siku 19 kutokana na pingamizi la dhamana lililowasilishwa na jopo la mawakili wa Jamhuri.

Alipandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, Septemba 19, 2024 akituhumiwa kwa mashtaka mawili likiwamo la kuchapisha taarifa za uongo katika mtandao wa kijamii.

Upande wa Jamhuri uliwasilisha pingamizi la Jacob kutopewa dhamana kwa madai ya usalama wake, kabla ya kutolewa kwa uamuzi wa pingamizi hizo, Jamhuri iliwasilisha tena maombi mengine mapya ya kiapo cha ziada katika kesi hiyo.

Akitoa uamuzi huo mdogo, Hakimu Kiswaga alisema, kiapo cha RCO wa Mkoa wa Polisi Kinondoni, Davis Msangi hakina maelezo ya ziada ya kutosha kuzuia dhamana hiyo.

Alisema sababu zilizotolewa hazina maelezo ya ziada ya kwanini mahakama isitoe dhamana, kwamba iwapo mjibu maombi ametoa maelezo ya usalama wake alitegemea mwombaji (Jamhuri) kupeleka uthibitisho wa maelezo ya mjibu maombi (Jacob).

Kutokana na hali hiyo, Mahakama ilikubaliana na maombi ya utetezi, mjibu maombi atapewa dhamana kwa mujibu wa masharti yatakayowekwa na mahakama hiyo, kwa hiyo inatupilia mbali pingamizi la upande wa Jamhuri la kuzuia dhamana.

Hakimu Kiswaga alisema ili mshtakiwa awe nje ya dhamana anatakiwa awe na wadhamini wawili wenye barua za Serikali za Mitaa na pia watatia saini bondi ya Shilingi milioni saba kila mmoja.

Hata hivyo, Jacob ametakiwa asitoke nje ya nchi bila kibali cha mahakama na ametimiza masharti hayo na kuachiwa huru. Kesi imeahirishwa hadi Oktoba 21, 2024 kwa ajili ya kutajwa na upelelezi haujakamilika.

Kabla ya kutolewa uamuzi huo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Job Mrema, alidai mahakamani kuwa wana maombi madogo yasikilizwe kwanza kabla ya uamuzi.

Hata hivyo, Wakili wa Jacob, Peter Kibatala alipinga hoja hiyo na kuiomba mahakama isikubali kuendeshwa na watu ambao hawajazingatia taaluma.

Baada ya hoja hizo, Hakimu Kiswaga alikataa hoja hiyo ya Mrema na kusema kuwa dhamana ni haki ya kikatiba ya mtu kupewa, wasubiri kwanza atoe uamuzi kama wana hoja zingine basi zije baadaye.

Jacob, anatuhumiwa kwa mashtaka mawili likiwamo la kuchapisha taarifa za uongo katika mtandao wake wa kijamii.

***Imeandikwa na Grace Gurisha na Grace Mwakalinga**

## HABARI KITAIFA

# Mpina amtwisha Nchimbi kero za wafugaji, wakulima

**Na Halfani Chusi,** MEATU

MBUNGE wa Jimbo la Kisesa (CCM), Luhaga Mpina, jana ameibua kero tatu za wakulima na wafugaji, akimtaka Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi kuitaka serikali kuzitatua ili wananchi wapate haki yao.

Kero hizo ni wafugaji waliokamatiwa mifugo yao kushinda kesi, lakini hadi sasa haijarejeshwa, wakulima kutozwa Sh. 300 katika kilo moja ya pamba kwa ajili ya kugharamia pembejeo na kilo moja ya mbegu kuuzwa Sh. 10,000 hali inayowakosesha haki wakulima.

Alisema wafugaji ambao mifugo yao ilitaifishwa na kushinda kesi mahakamani miaka mitatu iliyopita, mpaka leo hawajalipwa.

Mpina aliyasema hayo jana mjini Meatu mkoani Simiyu.

Akijibu hoja hizo, Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, alisema hatovumilia jambo lolote litakalofanywa kinyume cha sheria na viongozi wa serikali kwa kuwa yeye ni muumini wa utawala wa sheria.

"Nitalibeba suala hilo mpaka nihakikishe haki yao imepatikana kama walishinda kesi mahakamani hatupaswi kuwakimbia," aliahidi Nchimbi.

Mpina pia, alilalamikia kuwapo kwa wakulima wa pamba wanaokatwa Sh. 300 kwa ajili ya viwatilifu na kuuziwa mbegu ya mahindi kwa Sh. 10,000 kwa kilo.

Kutokana na hoja hiyo, Nchimbi alimtaka Mkuu wa Mkoa Simiyu, Kenani Kihongosi kujibu hoja hiyo na kusema: "Serikali inakwenda kutoa ruzuku mbegu za mahindi na watapata mbegu kwa bei nafuu."

"Suala la pamba nimelibeba na wataenda kuangalia namna ya kutatua changamoto hiyo na kwamba serikali kwa kushirikiana na Bodi ya Pamba wanaendelea kuangalia namna ya kumaliza tatizo hilo," alisema Kihongosi.

Aliwatuhumu baadhi ya wanasiasa kupewa mbegu kuzigawa kwa wakulima, lakini walikuwa wanampa kila mwananchi na asiye mkulima jambo lililochangia wengi kukosa.

"Hawa wanasiasa tumepiga marufuku endapo tutabaini hilo tena awe ni diwani au mwenyekiti tutachukua hatua za kisheria," alisema.

Hata hivyo, Mpina hakuridhika na majibu hayo na kunyoosha mkono, na alipopewa nafasi na Nchimbi alisema alichokisema mkuu huyo wa mkoa kuhusu wanasiasa kugawa mbegu sio kweli na kwamba hakuna viongozi wa siasa waliofanya hivyo.

**"Suala la pamba nimelibeba na wataenda kuangalia namna ya kutatua changamoto hiyo na kwamba serikali kwa kushirikiana na Bodi ya Pamba wanaendelea kuangalia namna ya kumaliza tatizo hilo," alisema Kihongosi.**

Aidha, alisema msimamo wake anataka kujua kwanini mbegu ya mahindi iuzwe kilo moja kwa Sh.10,000 na kipi kisababishi cha kufikia bei hiyo.

"Kuwasingizia wanasiasa ni kuwasingizia tu hakuna mwanasiasa anayegawa mbegu, aseme ni mwanasiasa gani ambaye huwa anasimama kugawa mbegu maana hili la mwanasiasa limekuwa kama haramu," alisema Mpina huku akishangiliwa na wananchi waliokuwa wamefurika eneo hilo.

Nchimbi akijibu, alisema chama chake kitaendelea kutetea wananchi wanyonge na kuwashirikisha katika masuala yote muhimu.

Aidha, alisema wananchi na viongozi wengine wanapaswa kumzoea Mpina akikumbushia alikuwa mbishi tangu wakiwa chuo wanasoma.

Akiwa Bariadi juzi, Nchimbi alisisitiza umoja, amani na mshikamano na kwamba hiyo ndio njia ya kuliunganisha taifa.

"Watanzania wa vyama vyote tunapaswa tujue jambo ambalo tulilonalo lenye thamani kubwa ni amani, umoja, mshikamano wa taifa letu," alisema Nchimbi.

Aidha, alisema kila anayejaribu kuvuruga umoja aambiwe kwa macho makavu kwamba hatupo tayari kuvumilia nchi iingie katika machafuko.

Akizungumzia miradi mikubwa ya maendeleo iliyofanikiwa ikiwamo Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR), mradi wa kufua umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, alisema hakuna mtu aliyeamini kwamba baada ya kuondoa Rais Dk. John Magufuli hakuna mtu atakayeweza kuumaliza.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameonesha kwa vitendo kuwa anapenda watu wake kwa kuhangaika kutafuta fedha za miradi ya maendeleo na kusimamia kuhakikisha inatekelezwa.

"Kwa hiyo kazi tuliyonayo ni ya kuendelea kumuunga mkono ili aendelee kuitumikia nchi yetu kwa uaminifu, upendo mkubwa na nchi yetu iendelee kupata maendeleo," alisema Nchimbi.

Kuhusu uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Katibu wa NEC, Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla, alisema chama hicho kitatumia mfumo wa KKK (Kuhamasisha, Kujiandikisha na Kuweka Mawakala).

Aidha, alitoa wito kwa wananchi ifikapo Oktoba 11 hadi 20, mwaka huu, wajitokeze kwa wingi kujiandikisha katika daftari la mkazi ili waweze kushiriki katika uchaguzi huo na kwamba chama kitaleta wagombea wenye sifa.

# Pindi azindua utalii wa puto Hifadhi ya Ruaha

**Na Francis Godwin,** IRINGA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii Balozi, Dk. Pindi Chana, amehitimisha kilele cha maadhimisho ya miaka 60 ya kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kwa kuzindua utalii wa puto.

Uzinduzi huo umefanyika jana katika eneo la Korongo View ndani ya Hifadhi ya Taifa Ruaha, mkoani Iringa.

Akizungumza baada ya uzinduzi huo, Dk. Chana alisema mafanikio hayo ni kutokana na jitihada za Rais Dk. Samia Suluhu Hassan za kutangaza vivutio vya utalii.

"Tunamshukuru Rais Samia kwa kuionesha dunia vivutio vya utalii vya Tanzania ambapo mpaka sasa watalii wameongezeka na kufikia milioni 1.8 na mapato ya Taifa tunachangia asilimia 17 na fedha za kigeni takribani Dola za Kimarekani bilioni 3.6.

Kuhusu maboresho ya miundombinu katika Hifadhi ya Taifa Ruaha, Dk. Chana alisema kuwa hadi sasa kuna barabara ya Iringa-Msembe yenye urefu wa kilomita 104 ambayo inaenda kujengwa.

Alisema katika Hifadhi ya Taifa Ruaha kutakuwa na uwanja wa ndege sambamba na kutumia uwanja wa ndege wa Nduli ulioko Mkoa wa Iringa ambao unaendelea kukarabatiwa.

Aidha, alisema kwa miaka mitatu kumekuwa na mabadiliko makubwa ya sekta ya utalii na serikali inazidi kuboresha maeneo mengi ya utalii huku akihamasisha wawekezaji kujitokeza kuwekeza katika hifadhi hiyo ya Ruaha.

Alisema Wizara ya Maliasili na Utalii inafanya kazi kubwa kusimamia hifadhi zote 21 nchini kuona zinaendelea kuwa tegemeo kubwa kwa taifa.

Alisema wizara hiyo ipo kutekeleza 4R za Rais Dk. Samia na ndio maana hailali inapiga kazi.

Kuhusu Hifadhi ya Ruaha, alisema ni moja kati ya hifadhi kongwe nchini na mafanikio makubwa yameonekana kupitia miaka 60 ya kuanzishwa kwake.

Alisema hifadhi za taifa zinatoa mchango mkubwa kwa taifa kwenye nyanja mbalimbali na kuwa Pato la Taifa limekuwa likichangia kwa kiasi kikubwa kupitia sekta hiyo.

Akizungumza kwa niaba ya wahifadhi wastaafu wa hifadhi hiyo, Loriviole Moirana, waliitaka serikali kuendelea kuikumbuka hifadhi hiyo kwa kutenga fedha za uendeshaji na kuzituma kwa wakati ili ziweze kusaidia kuendesha hifadhi pia kuwe na ndege zaidi ili kusaidia kupambana na matukio ya ujangili pamoja na uendeshaji wa hifadhi.

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Peter Serukamba, alisema Hifadhi ya Ruaha ni muhimu ambayo imefanya mkoa kuendelea kutangazika kupitia utalii.

Alipongeza wadau mbalimbali wa utalii ikiwamo kampuni ya Foxes ambao ndio waasisi wa utalii katika hifadhi hiyo.

Alisema kupitia jitihada za wadau wa utalii, hifadhi hiyo imepiga hatua kwa kuanzisha utalii wa puto.

Pia, alisema serikali imeendelea kufanya jitihada kubwa kwa kufungua utalii kwa kupitia filamu ya The Royal Tour pamoja na mradi mkubwa wa Regrow ambao unajenga viwanja vya ndege viwili; kiwanja cha Iringa na kiwanja cha Msembe pamoja na ujenzi wa lami kilomita 104.

## TAARIFA KWA UMMA.

### ZUIO (CAVEAT EMPTOR) – PLOT NO. 278 BLOCK "H" BOMANG'OMBE, HAI DISTRICT

1. Taarifa inatolewa na Kampuni ya Mwananchi Engineering And Contracting Company Limited (inayojulikana kama MECCO) kuujulisha umma kuwa tangazo lililotolewa na kuchapishwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai mnamo tarehe 1 Mwezi wa 10 Mwaka 2024, akiwakaribisha wananchi kununua viwanja katika eneo liliosajiliwa kama kiwanja namba "278" kitalu "H" katika eneo la Kijiji cha Sanya juu (linalofahimika kwa jina maarufu kama **"ENEO LA MECCO"** ni tangazo lisilo halali. Tangazo hilo sio tu kwamba linapotosha umma lakini pia ni ukiukwaji wa taratibu za Mahakama ambapo mwananchi atakayeshiriki kununua viwanja hivyo atapata changamoto za kiuchumi na kupelekea kupoteza fedha zake

2. Kwamba, umma unataarifiwa kutambua kwamba eneo hilo limepimwa na kusajiliwa kama Industrial Plot NA. "278", Kitalu "H", Registered Plan na. 34730 ya tarehe 12/02/2002 kwa mujibu wa Master Plan ya Mji wa Bomangombe, Kiwanja ambacho kinamilikiwa na **M/S. MECCO** kuanzia mwezi wa Januari, 2004 mpaka hivi leo. Kampuni ya MECCO imewekeza kiasi kikubwa cha pesa pamoja na kuendeleza eneo hilo kwa matumizi ya ujenzi wa viwanda yaliyokususudiwa kwa mujibu wa Mipango Miji (Town Master Plan).

3. Kwamba, tarehe 9 mwezi wa September, 2024 kwa barua yenye kumb namba LG /J. 10.1.12 Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai bila uhalali wowote na bila kujali taratibu za kisheria alitishia kuchukua eneo hilo kutoka kwa mmiliki halali ambaye ni **M/S MECCO.**

4. Kwamba, mnamo tarehe 17 mwezi wa September, 2024, MECCO alifungua kesi katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Moshi, ambayo ilisajiliwa kama maombi madogo namba 23327 ya mwaka 2024 (Misc. Land Application no. 23327 of 2024) dhidi ya Mkurugezi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kesi hiyo ipo mbele ya Mahakama Kuu Kanda Moshi na imepangwa kusikiliza tarehe 16.10.2024, na kwamba Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai ametaarifiwa ipasavyo.

5. Kwa mujibu wa taarifa hii mwananchi atakayeshiriki kununua viwanja hivyo hataweza kujitetea kwamba yeye ni ***"mnunuzi mwaminifu"*** (bonafide purchaser) na madai yake hayatatiliwa maanani. Kwamba, onyo linatolewa kwa umma kutojihusisha, au kununua, au kufanya kitu chochote kuhusiana na tangazo la ununuzi wa viwanja hivyo kwenye Kiwanja namba "278" Kitalu **"H" (ENEO LA MECCO)** lililotolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai.

**MAUNGO OBADIAH KWABHI.**
**MWENYEKITI, MWANANCHI ENGINERING AND CONTRACTING COMPANY LIMITED**

# Mwinyi aziagiza taasisi kushughulikia kero za wazee

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi ameziagiza taasisi zote zinazotoa huduma za ustawi kwa wazee, kuzishughulika haraka na kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazowakabili wazee hao.

Dk. Mwinyi alitoa agizo hilo Wilaya ya Chake, Mkoa wa Kusini, Pemba kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wazee, Duniani.

Taasisi zilizopewa agizo hilo ni Wizara ya Afya ambayo imeagizwa kuandaa madirisha maalumu hospitali zote ya kutoa huduma za wazee kwa kuwapa kipaumbele, pamoja na kuongeza madaktari bingwa wa magonjwa ya wazee.

Pia, ameiagiza Wizara ya Uchukuzi na Mawasiliano kuishughulikia Sheria vya Vyombo vya Barabarani na kuharakisha mchakato wa kuwapatia wazee vitambulisho maalumo vitakavyowasaidia kulipa nusu nauli kama ilivyo kwa wanafunzi na watu wenye ulemavu.

Wizara ya Fedha imeagizwa kuandaa bajeti maalumu ya kuendesha mabaraza ya wazee pamoja na kufungua madirisha maalumu kwenye benki na huduma za fedha yatakayotoa msaada na kipaumbele kwa kuwahudumia wazee hao.

Rais Dk. Mwinyi, pia ameitaka Wizara ya Wanawake, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana taasisi na jumuiya zinazoshughulika na masuala ya wazee nchini kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuepukana na mitazamo potofu kwa kuwapachika wazee tuhuma za uchawi.

Amesema, serikali imeandaa na inaendelea kutekeleza Sera ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2014 ambayo imeweka mikakati madhubuti ya kusimamia maendeleo ya wazee. Kadhalika, serikali imetunga Sheria ya Masuala ya Wazee namba 2 ya mwaka 2020 kwa maadhimisho ya kusimamia haki na maslahi ya wazee nchini.

Pia, Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Jumuiya na Mabaraza ya Wazee katika ngazi ya Mkoa, Wilaya na Shehia inafanya kila juhudi kusimamia na kuimarisha maendeleo ya wazee nchini.

Alisema hadi sasa shehia na wilaya zote nchini zimeanzisha mabaraza ya wazee. Kwa hakika, hii ni hatua kubwa kwani mfumo huu wa kuwepo mabaraza kuanzia ngazi ya chini kabisa unasaidia katika kupeleka taarifa kwa wepesi na kurahisisha utatuzi wa changamoto pale zinapotokezea.

Akizungumza kwenye maadhimisho hayo ya Siku ya Wazee Duniani, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, amesema Serikali ya Mapindizi ya Zanzibar itaendelea kuwapa Wazee maisha yenye heshima kama wanavyotambulika kwenye Katiba zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ya Zanzibar.

Akisoma risala kwa niaba ya Wazee wenziwe, mwakilishi wa wazee, Ali Said Mattar, ameiomba serikali kuwapa kipaumbele kwenye huduma za afya, usafiri, na benki kwa kuwaharakishia mchakato wa kuwapatia vitambulisho maalumu vitakavyowatambulisha sehemu hizo pamoja na kuwapatia nafasi maalumu za uwakilishi kwenye vyombo vya kutungia sheria ikiwamo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza wa Wawakilishi ili kuzisemea changamoto zinazowakabili.

Aidha, Wazee hao wameiomba Serikali kuifanyia marekebisho Sheria ya usafiri wa vyombo vya barabarani, namba 7 ya mwaka 2007 kwa kuwatoza nusu nauli wazee wote kwenye usafiri wa umma kama ilivyo kwa wanafunzi na watu wenye ulemavu.

Pia wamempongeza Rais Dk. Mwinyi kwa kuwaongezea Wazee pensheni Jamii kutoka elfu 20 hadi 50 na pensheni ya wastaafu kutoka elfu 90 hadi laki moja na 80.

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Kimataifa "HelpAge" Smart Smart Daniel, ameisifu Serikali ya Mapindizi ya Zanzibar kwa kuendelea kuwajali, kiwathamini na kuwatunza Wazee kwa kutumia gharama kubwa zaidi ya bilioni 17. 6 kwaajili ya kulipia pensheni Jamii suala alilosema kuwa Zanzibar ni nchi ya kwanza duniani kwa Serikali kutumia gharama kubwa kwa Wazee bila ya misaada kutoka nje au mashirika ya kimataifa.

Siku ya Wazee duniani ilianza kuazimishwa mwaka 1991 na Tanzania hususani Zanzibar ilianza mwaka 2004 na ujumbe mahusisi kila mwaka, ujumbe wa mwaka huu ni "kuzeeka kwa heshima; umuhimu wa kuimarisha matunzo na mifumo ya usaidizi kwa wazee".

# 'Wafanyakazi wanatakiwa kuwa na washauri kulinda afya ya akili'

**Na Christina Mwakangale**

IMESHAURIWA na wanataaluma wa afya ya akili kwamba, mahali pa kazi kuwapo 'mentors' (washauri), ili kuponya 'majeraha' ya kiakili kazini yanayowakumba wafanyakazi kama vile sonona na msongo wa mawazo.

Bingwa wa Afya na Magonjwa ya Akili, kutoka Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe (MNMH). Dk. Godwin Mwisomba, amesema takwimu za dunia zinaonesha mahali pa kazi ni eneo mojawapo la chanzo cha magonjwa ya akili.

"Utafiti wa Shirika la Afya Duniani (WHO), unaeleza kwenye kila wafanyakazi watano, mmoja wao ana 'work related stress' (msongo wa mawazo utokanao na kazi), na kusababisha magonjwa ya akili.

Pia kuna utafiti wa Deloitte wa mwaka 2022 unasema kwamba asilimia 84 ya wafanyakazi wamepitia changamoto za msongo utokanao na kazi ama mazingira ya kazi," alisema Dk. Mwisomba.

**"Utafiti wa Deloitte umegundua kwamba wazazi ambao wanajali afya ya akili ya mtoto wao walijikuta wakijitahidi kufanya vyema kazini na kuendeleza maisha yao ya nyumbani na kazini. Kazi hufanya sehemu kubwa ya maisha yetu."**

"Utafiti wa Deloitte umegundua kwamba wazazi ambao wanajali afya ya akili ya mtoto wao walijikuta wakijitahidi kufanya vyema kazini na kuendeleza maisha yao ya nyumbani na kazini. Kazi hufanya sehemu kubwa ya maisha yetu."

Dk. Godwin alisema sheria ya afya ya akili, bado haijaegemea katika masuala ya afya ya akili mahali pa kazi, ili kuweka masuala hayo kisheria, kama vile kutoa huduma ya kwanza ya afya ya akili iwapo kuna hitaji hilo kazini.

Alisema kuelekea Siku ya Afya ya Akili Duniani, kila jamii, mwajiri na mwajiriwa ni muhimu kuangalia wajibu wao, ili kulinda afya ya akili, kwa kuweka mazingira rafiki ya kufanyia kazi.

"Historia inaonesha ni suala muhimu katika elimu hii, inabidi tulizungumzie kwa sababu utafiti namba zinaonesha kuna tatizo kuhusu suala la afya ya akili mahali pa kazi.

Utakuta kuna watu wanafanya kazi mtandaoni, wapo wameajiriwa huko, je, bosi anakutreat vipi. Au kama umejiajiri mazingira yako yakoje? Labda unapokea matusi mtandaoni vyote hivyo vinahitaji kuzungumza kama kazi ya mtandaoni inakuletea kipato kuna tatizo, kuna haja ya kulizungumzia."

Mwanasaikolojia kutoka Hatua Therapies, Jestus August, alisema katika mahala pa kazi kumtambua mfanyakazi bora mbele ya hadhira ni jambo jema, ingawa kwa baadhi ya wafanyakazi huwa chanzo cha magonjwa ya akili kama vile sonona.

Alisema pia mahala pa kazi iwapo miongoni mwa wafanyakazi mwenzako amekukosea si vyema kumsema kwa watu, badala yake mhusika afuatwe kwa lugha ya kirafiki.

"Ni muhimu kuwa na 'mentors' washauri, kuna wakati mabosi wetu wanatukosea, wafanyakazi wenzetu wanatukosea, malipo hayaturidhishi hivyo ili kupona na kuwa na afya ya akili yenye utengamao kuna haja ya kuwa na 'mentors' hawa ni zaidi ya walimu ili kutuweka sawa," alisema mwanasaikolojia huyo. Alisema mahali pa kazi pia vijana huathiriwa zaidi, kama vile kuegemea katika ushabiki wa timu za michezo ya aina tofauti, huku wakitoa kauli zisizofaa kulingana na mazingira walioko, wakijisahau kwamba eneo hilo ni mahali pa kazi.

"Kuna ambao wanavaa tofauti mahali pa kazi, anaambiwa usivae viatu vua michezo yeye anavaa mahali pa kazi. Kingine ni kutamani kuweka malengo binafsi hasa kwa waliotoka vyuoni kutaka maendeleo ya haraka kuliko aliowakuta kazini.

Kijana anakuwa na matarajio makubwa kwamba anawaza awe na mshahara mkubwa, awe na safari nyingi za nje, apendwe sana na bosi, asafiri nje sana, hayo matarajio hayo yanamfanya atamani makubwa, asipopata mambo yanaharibika, anadhani kazi hii ndio italeta mafanikio kwa ukoo, familia yote, huku mshahara kidogo, unavuruga afya ya akili," alisema August.


## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

## TANGAZO LA MRADI WA VIWANJA ENEO LA KIKOMBO KITALU "DA" NA "N"

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE AMBAO HAWAJAKAMILISHA MALIPO YA UNUNUZI WA VIWANJA KATIKA MRADI WA VIWANJA ENEO LA KIKOMBO KATIKA KITALU "DA" NA "N" KUWA WANATAKIWA KUKAMILISHA MALIPO YOTE NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14) KUANZIA TAREHE 3 HADI 16 OKTOBA, 2024.


KUSHINDWA KUKAMILISHA MALIPO HAYO; KIWANJA HICHO KITATOLEWA KWA MWOMBAJI MWINGINE BILA TAARIFA ZAIDI KWAKO NA WEWE UTAREJESHEWA FEDHA YAKO BAADA YA KUKATWA ASILIMIA 10 KWA GHARAMA ZA USUMBUFU.

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA MKURUGENZI WA JIJI LA DODOMA**


SAKO Kwa BAKO
Pamoja kila hatua
Ahsante
1994 1995 1996 1997 1998 1999 2000 2001 2002 2003 2004 2005 2006 2007
miaka
2008 2009 2010 2011 2012 2013 2014 2015 2016 2017 2018 2019 2020 2021 2022 2023 2024
30
ya Huduma
4G+ kila kona
5G
tigo

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII




# Tusifanye mchezo ni muhimu kujua afya ya akili

**AFYA** ya akili ni sehemu muhimu ya mwili wetu, hivyo kuna umuhimu mkubwa wa kutunza afya yetu ya kimwili ili kuepuka kuwa na magonjwa makubwa.

Kwa mujibu wa wataalamu wa afya, kila mtu ana tatizo la afya ya akili na hii hujidhihirisha jinsi watu wanavyochukua maamuzi, wanavyoona, mawazo yanayokuja ni kwa sababu yanafanyika kutokana na kile kilicho akilini.

Wataalamu wanaeleza kuwa, afya ya akili huleta madhara mtu anapoamua kuzingatia "tatizo ni nini" badala ya "kile kilicho kizuri na kinachoendelea vizuri". Wengi wanaweza kujua dalili za magonjwa ya kimwili, kama vile mshtuko wa moyo au kiharusi, lakini hawajui afya mbaya ya akili.

Kwanini afya ya akili ni muhimu ni kwa sababu inaathiri mawazo, tabia na hisia. Kuwa na afya njema kihisia na kiakili kunaweza kukuza tija na ufanisi katika shughuli za kila siku za maisha. Pia ina jukumu muhimu kudumisha miunganisho ya kijamii, uhusiano na inaruhusu mtu kuzoea mabadiliko katika maisha na kukabiliana na shida.

Ndio maana kuna kila sababu ya watu kufahamu afya ya akili ili waweze kufanyakazi kwa tija.

Mambo madogo au hatua zinaweza kusaidia katika kuimarisha afya ya akili.

Wataalaamu wa afya wameelekeza njia chache za kukabiliana na tatizo mahususi la afya ya akili, kushughulikia hisia kali vizuri zaidi, au tu kujisikia chanya na mwenye nguvu zaidi.

Mambo yanayoshauriwa na wataalamu hao ni kufanya uhusiano wa kijamii kuwa kipaumbele, kulenga kwa dakika 30 za shughuli kila siku, kula chakula cha ubongo chenye uwiano na afya, kufanya wakati wa burudani kuwa kipaumbele, kukumbuka, kushukuru, kulenga

kwa saa saba hadi tisa za usingizi bora kila usiku, kutenga muda wa kutafakari (kutathmini upya) na kuthamini bila kupita kiasi.

Afya ya akili inaweza kuathiri watu tofauti kwa njia tofauti. Ikiwa juhudi zote za mara kwa mara za kuboresha afya hiyo na kihisia bado haisaidii ufanye kazi ipasavyo nyumbani, kazini au katika mahusiano yako, unaweza kuwa wakati wa kutafuta usaidizi wa kitaalamu.

Mtu anapoanza kuona mabadiliko katika furaha na mahusiano yao kwa ujumla, daima kuna njia chanya za kupata chakula kinachohitajika.

Baadhi ya njia za kupata usaidizi ni kuunganishwa na marafiki na familia, ambayo inapendekezwa kufikia watu maishani ambao wanaweza kusaidia kutoa msaada wa kihemko.

Kujifunza juu ya afya ya akili, hapa inaelezwa kuwa kuna nyenzo nyingi ambazo mtu anaweza kugeukia kwa kujifunza zaidi kuhusu afya ya kihisia.

Aidha, kutafuta msaada wa kitaalamu, hasa kwa mwanasaikolojia au mtaalamu wa magonjwa ya akili na kupata usaidizi wa kibinafsi mtu anaoutaka.

Afya ya akili inaweza kuathiriwa na mambo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na matukio ya maisha au hata maumbile yako. Hatimaye, afya ya akili ni hali ya ustawi na si tu kutokuwapo au kuwapo kwa hali ya afya ya akili.

Wataalamu wanaeleza kuwa mtu anapokuwa na hasira nyingi, sio dalili nzuri hivyo inampasa kwenda kumwona mwanasaikolojia ili aweze kumsaidia kwa sababu ni moja ya dalili ya kuwa na afya ya akili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Hongera Dira 2050 kubeba maoni ya watoto

**WAZIRI** wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amepokea maoni ya watoto kuhusu Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050. Anayapokea maoni yao hivi karibuni, jijini Dar ss Salaam, ikiwa na mambo mengi lakini la kuwapongeza ni hili hawakusahau wale wanaoishi na ulemavu.

Watanzania hao wadogo wanataka kuboreshwa huduma za watoto wenye mahitaji maalum ili nao wafurahie haki za msingi za kila binadamu.

Wanataka watoto ambao wanatakiwa kuwa shuleni wapate haki hiyo, pia kuimarishwa kwa afua za kupambana na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto ambavyo sasa vinaumiza jinsi zote.

Vilevile, wanatamani kutokomezwa kwa mila na desturi zenye madhara kwa watoto katika jamii, kutokana na ukweli kwamba vitendo hivyo vimekuwa vikiendelea kuripotiwa kila mara vikitokea maeneo mbalimbali.

Watoto wanaelezea mengi kuhusu dira hiyo, na wanataka kuwapo haki ya mtoto ya kushiriki kwenye masuala yanayowahusu kwa kuangalia umri wao. Wanaomba ushiriki katika masuala yanayohusu haki na ustawi wao ikiwa ni pamoja na dira yao ya maendeleo ya watoto.

Kwa ujumla maoni ya watoto yanagusa maeneo ya uboreshaji wa miundombinu ya elimu, afya na usafirishaji, uwapo wa wataalamu wa kutosha wa afya na ongezeko la idadi ya walimu na kuboreshwa kwa mitaala na mbinu za kutoa na kupata elimu katika shule za msingi na sekondari.

Kwa kuwa kumekuwapo na kelele nyingi za kutaka watoto kulindwa dhidi ya matukio ya hatari na pia kusaidiwa kupata elimu, ni vyema maoni yao yakafanyiwa kazi ili kupunguza changamoto zinazowakabili.

Maeneo kama kuboreshwa kwa huduma za watoto wenye mahitaji maalum hasa wale wanaotakiwa kuwa shuleni na kuimarishwa kwa afua za kupambana na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto sambamba na kutokomeza mila na desturi zenye madhara kwa watoto katika jamii, ni ya muhimu kwa ustawi wao.

Ninaamini kuwa kuwashirikisha watoto katika dira hiyo ni kuwaandaa kuwa tayari kuongoza na kuitekeleza. Ni udhihirisho kuwa ni dira jumuishi na inayobeba karibu raia wote bila kujali ni wadogo au wakubwa.

Hivyo, kuwaruhusu kutoa maoni na hata kuyafanyia kazi, kutasaidia kuongoza kundi la watoto katika kutimiza matarajio yao hasa maoni ambayo wameyatoa kwenye dira hiyo.

Kimsingi mchakato wa kukusanya maoni una lengo la kufikia malengo muhimu ya kuwajenga watoto na kuwaandaa kama nguvu kazi na uwezo wa kufanya maamuzi kwa wakati ujao.

Kwa maana hiyo, kufanyia kazi maoni yao ni jambo la msingi ili sauti zao zisikike kama ambavyo inafanyika kupitia maoni ya makundi mengine.

Ikumbukwe kuwa watoto wanakabiliwa na ukatili wa kila aina, wengine hawana fursa ya kupata elimu, lakini hata wale wanaosoma, wanakabiliwa na vikwazo vingi shuleni.

Ni kawaida kukuta baadhi ya shule hazina vifaa cha kujifunzia na kufundishia, uhaba wa walimu, madawati na miundombinu mingine muhimu kwa ajili yao.

Hivyo, kwa kuwa wamepewa fursa ya kutoa maoni, basi ni vyema wakasikilizwa ili nao watambue kuwa wanathaminiwa na serikali yao.

Watoto wengi pamoja na changamoto hizo ni waathirika wa matatizo ya afya ya akili. Kama taifa kuna huduma za kuwasaidia kuanzia wataalamu, miundombinu, tiba na kuwarejesha tena kwenye mafunzo ikizingatiwa kuwa umri wao ni mdogo na wanahitaji kusonga mbele.

Ni mambo ya kuangalia kwenye dira inayoandaliwa ili watoto ambao idadi yao ni kubwa wasiwe wasikilizaji bali wachangiaji, wachambuzi, watoa hoja na mapendekezo kwenye ajenda za maendeleo ya taifa.

# RC adhibiti utoroshaji mtoto kwenda kutumikishwa

**Na Vitus Audax**

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Paul Chacha amedhibiti mpango wa utoroshaji wa mtoto kutoka wilayani Ngara mkoani Kagera kwenda Dar es Salaam, anayedaiwa kuachishwa masomo na kusafirishwa kinyemela na mawakala wa usafirishaji watoto wakidai kuwa wanampeleka kufanyakazi.

Chacha alibainisha hayo jana baada ya kumpata mtoto huyo aliyekuwa akisafirishwa katika moja ya mabasi yaendayo jijini Mwanza ambalo lilitakiwa kwenda kituo cha polisi baada ya kupokea taarifa za kuwapo kwa mtoto anayesafirishwa kinyume cha sheria.

"Nilipata taarifa kutoka kwa raia wema juu ya kitendo cha mtoto mdogo kusafirishwa kutoka Ngara mpaka Kahama kwa kutumia watu wanaosafirisha watoto kwa kusema wanaenda kufanya kazi, watu hawa wanajiita mawakala," alifafanua Chacha.

Alisema mtoto huyo mwenye umri wa miaka 13 ambaye kimsingi alikuwa hajui anakopelekwa na watu hao, baada ya mazungumzo alisema anatokea Ngara na waliokuwa wanamsafirisha walimlaghai kwamba wanampeleka kwa shangazi yake Kahama.

Alisema baada ya kufika Kahama akafaulishwa kwenye gari ambayo inaelekea Dar es Salaam ambako baada ya mtoto huyo kuona amepitishwa eneo alipotaka kwenda, alianza kulia ndani ya basi na kusababisha baadhi ya abiria wasamaria wema kutoa taarifa na gari hilo kutakiwa kwenda polisi.

"Abiria mtatusamehe sana kwa kuwasumbua na kuwaleteni kituoni hapa lengo letu lilikuwa ni jema na pengine ninyi msinge kubali kuona mtoto anasafirishwa kwenda kufanyishwa kazi, lakini tofauti na kazi pengine kuna mambo mengine wanawafanyia ambayo sisi hatuyajuhi," alisema Chacha.

Aidha, alisema vitendo vya namna hiyo hawezi kuvifumbia macho, mtoto mdogo anakatishwa masomo yake na watu wenye nia ya kujipatia pesa kwa njia hizo ovu.

Chacha alisema wahalifu wote wanaofanya vitendo mbalimbali vya kihalifu wanatakiwa wafahamu Tabora sio sehemu salama yakufanya vitendo hivyo, vyombo vya ulinzi na usalama katika mkoa huo viko makini.

Alisema wanaendelea kuwafuatilia wote waliokuwa kwenye mnyororo huo wa kumsafirisha mtoto huyo na kuahidi kuwapata wote kisha kuwafikisha mahakamani na kuwa taratibu za kumrejesha mtoto huyo nyumbani kwao zinaendelea.

Alisema mawakala wote watawakamata ili wavieleze vyombo vya sheria kuwa masuala hayo yana maana gani kwa matukio ya watoto kupotea na kukutwa wamechinjwa na kuondolewa baadhi ya viungo yamekuwa mengi nchini na kwamba vitendo hivyo vinaashiria kuwa ni wahusika wakubwa wa matukio hayo.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Alhaji Jabiri Shekimweri (kushoto), akishiriki mchezo wa kukuna nazi kwenye bonanza lililofanyika juzi Uwanja wa Dodoma Sekondari kwa ajili ya kuhamasisha wananchi kujitokeza kwenye uandikishaji wa daftari la mpigakura ili kushiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika Novemba 27, mwaka huu. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# TCRA: Wananchi lindeni taarifa zenu mtandaoni

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imewataka wananchi kuongeza umakini kwa kulinda taarifa zao katika wakati wa uchumi wa kudijitali ambao huduma nyingi zinafanyika kwa mtandao.

Imesema usalama wa mtandao ni muhimu zaidi kuliko kipindi cha nyuma kwa kuwa huduma za benki hadi burudani zinafanyika kwa mtandao.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam wakati akizungumzia umuhimu wa usalama mtandaoni katika dunia ya kidijitali na namna Watanzania watakavyofikia malengo ya kiuchumi.

TCRA imezindua kampeni kabambe ijulikanayo "Ni Rahisi Sana" inayolenga kuelimisha wananchi namna ya kubaini na kutambua matapeli na wezi mtandaoni.

"Kampeni hii inalenga maeneo mengi ambapo itaiendesha kote nchini kuinua kiwango cha uelewa wa umma kuhusu fursa za mtandao wa intaneti na usalama wake. Kampeni hiyo ya awamu mbili itatekelezwa kati ya Oktoba na Desemba 2024, na Januari na Machi 2025 mtawalia, TCRA itatoa mbinu na maarifa ya usalama mtandaoni," alisema.

Dk. Bakari alisema TCRA itakuwa na watu binafsi na taasisi zaidi kutumia kikoa cha Tanzania kwenye tovuti zao na anwani za barua pepe.

"Kampeni pia inahusisha namna ya kugundua maudhui mitandaoni yanayolenga kupotosha, na pia jinsi ya kugundua habari feki. Walengwa watafundishwa pia njia za kutoa taarifa za uhalifu mtandaoni," alisema.

Vilevile, alisema kampeni inaendeleza uelewa wa wadau kuhusu klabu za kidijiti na ubunifu, na imeanzisha na inaratibu uanzishaji wa klabu za kidijiti ili kuendeleza uelewa wa masuala ya kidijiti kuanzia ngazi ya elimu ya chekechea hadi vyuo vikuu.

"Ubunifu na ulinzi wa wadau ni mojawapo ya masuala muhimu yanayosisitizwa kwenye mpango mkakati wa TCRA unaotelekezwa kati ya mwaka wa fedha 2021/2022 na 2025/2026," alisema.

Dk. Bakari alisema TCRA imeandaa ujumbe mahsusi kwa kila eneo la kuongeza elimu na ujumbe utatolewa kupitia vyombo vya habari, meseji fupi kwenye simu za mkononi na kwenye maeneo ya umma ikiwa ni pamoja na mabasi, treni na vivuko.

Aidha, alisema ingawa mipango ya kuongeza uelewa wa umma ni ajenda ya kudumu ya TCRA, kampeni hiyo inatokana na umuhimu wa kipekee kuwapatia Watanzania mbinu za kujilinda dhidi ya mashambulio ya mitandao ya intaneti na simu. Alisema TCRA inajitahidi kuelimisha umma kuhusu usalama na uimara wa mitandao na matumizi bora, wananchi wanahimizwa kutuma kwa ujumbe mfupi, wapatapo namba ya tapeli kwenda namba "15040" huduma ni BURE.

"Kuendeleza elimu ya masuala ya kidijiti na usalama mtandaoni kunahakikisha kuwapo mazingira salama na imara ya matumizi ya mitandao," alisema.

Kampeni hiyo inatokana na mpango mwingine wa TCRA kuhamasisha watu na taasisi kutumia kikoa cha Tanzania, yaani dot tz kwenye tovuti zao na anwani za barua pepe.

Mkurugenzi alisema mpango huo ulieleza faida za kikoa cha Tanzania, ikiwa ni pamoja na tovuti husika kupatikana kwa urahisi wahusika wanapotafuta vitu au huduma zinazotolewa na watu au kampuni za Tanzania.

"Matumizi ya kikoa cha Tanzania pia yanaonesha weledi wa mwenye tovuti na pia inatoa fursa za kujitangaza na kujijenga kibiashara. Vilevile yanajenga imani ya watumiaji wa huduma husika na kuwezesha mwenye kikoa kupanua wigo wa wateja," alisema.

Kampeni hii ya sasa imezinduliwa mwezi mmoja baada ya ripoti ya Shirika la Mawasiliano Ulimwenguni (ITU) kuitaja Tanzania kama mojawapo ya vinara 46 wa usalama mitandaoni kwa mwaka 2023. Kwa mujibu wa ripoti hiyo ya ITU, inayoitwa Fahirisi ya Dunia ya Usalama mtandaoni, Tanzania inaongoza nchi za Mashariki na Kati mwa Afrika kwa viwango vya juu vya usalama mitandaoni.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# GGML yatumia bilioni 1.8/- kujenga nyumba za polisi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Uchimbaji Madini ya Geita (GGML) imetumia zaidi ya Sh. bilioni 1.8 kujenga nyumba sita za maofisa wa polisi mkoani Geita, ikiwa ni sehemu ya uwajibikaji wa kampuni kwa jamii (CSR).

Kujengwa kwa nyumba hizo kumelenga kutoa makazi ya kisasa kwa maofisa wa polisi na kuimarisha utendaji kazi wa jeshi hilo pamoja na kuwafanya wafanye kazi kwa ufanisi na kuchangia ulinzi na usalama kwa wananchi.

Akizungumza juzi wakati wa hafla ya makabidhiano ya nyumba hizo, Makamu wa Rais wa Anglogold Ashant anayeshughulika na masuala ya uendelevu na mahusiano Afrika, Simon Shayo, alisema bila usalama hakuna mtu wala biashara inayoweza kufanikiwa.

Alisema uamuzi wa kusaidia vyombo vya dola umelenga kuchangia katika jamii yenye amani na ustawi na kwamba ubia baina ya polisi na mgodi umesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza matukio ya uhalifu kwa watu waliokuwa wakiingia mgodini bila kibali.

Aidha, kupitia ubia huo, wameanzisha polisi jamii na kufanya kuwa ubia wa mfano.

"Tulichokifanya hapa tumeanza kujaribu kukifanya kwa nchi nyingine tunazofanya kazi tunahangaika na matukio ya uhalifu na unavyofahamu huwezi kuwa na mgodi salama kama jamii inayokuzunguka sio salama," alisema Shayo.

"Usalama wetu na wa watu wanaoishi karibu na shughuli zetu ni muhimu sana na tunajivunia kuwa washirika katika kuhakikisha ustawi wao majukumu yetu kama kampuni inayo wajibika tunaenda mbali zaidi ya uchimbaji madini yanayohusisha ushiriki wa moja kwa moja katika ukuaji wa jamii na umma kwa ujumla," alisema Shayo.

Alisema mgodi huo umejikita kufanikisha malengo ya maendeleo ya Tanzania, na kuona hatua kama hiyo ni njia ya kusaidia juhudi za serikali katika kujenga jamii zenye nguvu, salama na zilizo na ulinzi.

"Tunafahamu usalama ni nguzo ya maendeleo, bila usalama hakuna mtu wala biashara inayoweza kufanikiwa kwa kusaidia vyombo vya dola, tunalenga kuchangia katika jamii yenye amani na ustawi," alisema Shayo.

Aidha, miradi mingine ikiwamo ujenzi wa ofisi pamoja na nyumba ya kuishi kamanda wa polisi mkoa, ujenzi wa vituo vya polisi jamii, ununuzi wa pikipiki 50 za askari kata pamoja na kufadhili mafunzo kwa vijana wanaoimarisha ulinzi kwenye vijiji vinavyozunguka mgodi kazi ambayo imesaidia kupunguza uhalifu kwenye mkoa huo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Saphia Jongo, alisema makabidhiano ya nyumba hizo ni uthibitisho wa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na wawekezaji.

Alisema kujengwa kwa nyumba hizo ni makubaliano kati ya Jeshi la Polisi na GGML na mradi huo utachangia kuimarisha utendaji wa maofisa na kuwafanya wafanye kazi kwa ufanisi na kuchangia ulinzi na usalama kwa watu.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Daniel Siro, akizungumza kwenye uzinduzi huo, aliitaka jamii hususan migodi kushirikiana na Jeshi la Polisi katika miradi ya kimkakati ya kuimarisha mifumo ya usalama ya raia na mali zao na kutunza utulivu wa nchi.

## Wakazi Mbwawa wapigania kupata kituo cha afya

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAKAZI wa Kata ya Mbwawa, Halmashauri ya Mji wa Kibaha wako kwenye mchakato wa kutafuta eneo la ujenzi wa kituo cha afya baada ya kuwa na zahanati pekee.

Diwani wa Mbwawa, Judith Muluge, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na Nipashe kuwa wamewashirikisha wananchi jambo hilo ili kusogeza huduma zaidi za afya kwenye kata hiyo.

Aliwaomba wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kupata eneo hilo kama ilivyo katika mambo mengine ya maendeleo ambayo wamekuwa wakitoa ushirikiano kuyafanikisha.

Uongozi wa kata hiyo pia unaendelea na mpango wake wa ujenzi wa bweni la Shule ya Sekondari Mbwawa kuwaondolea wanafunzi adha ya kutembea umbali mrefu.

Judith alisema Kata ya Mbwawa ina shule ya sekondari moja na kusababisha watoto wengi kutembea umbali mrefu kwenda shule na kukumbana na vikwazo vingi ikiwamo usafiri ambao mara nyingi daladala zinashindwa kubeba wanafunzi.

Akizungumzia kikwazo kingine kinachoikabili kata hiyo, Judith alisema bado kuna migogoro ya wakulima na wafugaji inayochangiwa na baadhi ya wafugaji kupitisha mifugo kwenye mashamba ya wakulima.

Alisema suala hilo linaendelea kutafutiwa ufumbuzi kwa kuwashirikisha wataalamu, na tatizo la wizi wa mifugo ambalo limekuwa likitokea katika kata hiyo.

Aliwaomba wananchi kuzingatia sheria na kila mmoja kuheshimu shughuli ya mwingine katika kukuza maendeleo kwa kuwa kitendo cha mifugo kuingia kwenye mashamba ya wakulima kinachangia njaa kwa baadhi ya wakulima kwa kukosa mavuno.

Katika hatua nyingine Katibu wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Pwani, Adam Mfilinge, aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa viongozi wanaochaguliwa kuhakikisha miradi inayoibuliwa inatekelezeka kama ilivyopangwa.




Mkurugenzi Mtendaji Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Dodoma (DUWASA), Mhandisi Aron Joseph, akikata utepe kuashiria uzinduzi rasmi wa maadhimisho ya huduma ya wiki ya wateja kwenye ofisi hiyo, jijini Dodoma jana, maadhimisho hayo yameanza jana yataendelea kwa mwezi moja. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali kutatua changamoto anazopitia mtoto wa kike

**Na Elizabeth Zaya**

KATIBU Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Amon Mpanju, amesema serikali, imejipanga kutatua changamoto zinazowakabili watoto wa kike nchini.

Alisema hayo hivi karibuni jijini Dar es Salaam wakati akiongea na waandishi wa habari kuhusu siku ya mtoto wa kike duniani inayotarajia kufanyika wilayani Bahi mkoani Dodoma, Oktoba 11, mwaka huu.

Mpanju alisema migogoro mingi inayotokea ngazi ya familia inachangia kwa kiwango kikubwa kuharibu malezi kwa watoto.

Alisema utafiti wa hali ya afya ya uzazi na mtoto pamoja na viashiria vya malaria ya mwaka 2022, iliainisha kwamba changamoto zinazowakabili watoto zimechangiwa kwa kiwango kikubwa na mifarakano na kutoelewana kwa ngazi ya familia inayosababisha malezi duni kwa watoto na kuwa katika hali hatarishi huku wengine kuanza kuingia kwenye mahusiano ya kimapenzi mapema kabla ya umri halisi.

Mpanju alisema taarifa hiyo inaonesha kwamba watoto wenye umri kati ya miaka 15 hadi 19 sawa na asilimia 27 walipata mimba za utotoni katika kipindi cha mwaka 2015/16.

"Na ilionesha kwamba hali ya mimba vijijini kwa watoto ni asilimia 25 ukilinganisha na asilimia 16 kwa watoto wa mijini, hivyo, watoto wetu wamekuwa wakikabiliwa na changamoto mbalimbali ndani ya jamii ikiwamo vitendo vya ubakaji, ulawiti, mimba na ndoa za utotoni," alisema Mpanju.

"Kwa mujibu wa taarifa ya makosa ya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji ya Jeshi la Polisi kuanzia Januari hadi Desemba 2023, matukio ya ukatili wa watoto yalikuwa 153,001 ukilinganisha na matukio ya vitendo vya ukatili vya watoto kwa kipindi hicho kwa mwaka 2022 ambayo yalikuwa 12,163 na mikoa ya kipolisi ya Arusha, Morogoro, Tanga, Kinondoni pamoja na mjini magharibi ndio ikiwa kinara."

Mwanafunzi kutoka Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) na Mjumbe wa Bodi ya Ushauri ya Wasichana kutoka Msichana Initiative, Letisia Mswaki, alisema wapo wasichana wengi wanaopata changamoto mbalimbali, lakini hawapati haki zao za msingi kutoka kwa watu au mamlaka za kutoa haki hizo.

Successfully Ufahama, mwanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Godwin Gondwe, kidato cha kwanza ambaye ni Mwenyekiti wa Klabu ya Flaviana Matata Foundation, alisema vijijini wasichana wengine wanakosa elimu kwa sababu ya umbali wa maeneo waliyopo ambayo pia yanachangia wakose elimu na hata kupitia na kuiomba serikali kuweka mazingira mazuri ya kumwezesha msichana kutimiza malengo yake ya kielimu.

Aidha, aliiomba serikali kuweka miundombinu mizuri shuleni ili kuokoa wasichana wanaokumbwa na ukatili kwa sababu ya kutembea umbali mrefu kwenda na kurudi shuleni ambao baadhi yao imekuwa chanzo cha kukatisha masomo na kuozeshwa mapema.



# Kongamano la kutangaza vivutio utalii kufanyika Z'bar

**Na Allan Isack**, ARUSHA

KAMISHENI ya Utalii Zanzibar (ZTC), inatarajia kufanya kongamano kubwa la kwanza la maonesho ya utalii kwa ajili ya kutangaza vivutio na fursa za uwekezaji zinazopatikana Zanzibar.

Hayo yalisemwa juzi na Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Arif Arbas Manji, wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Arusha.

Alisema tamasha hilo litafanyika kuanzia Oktoba 25, mpaka 26 mwaka huu kwa lengo la kutangaza vivutio vinavyopatikana kwenye visiwa hivyo vya marashi ya karafuu pamoja na fursa za uwezekezaji zilizoko huko.

"Tunakushuru Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, kwa kuwa ulituahidi kuwa tutashirikiana pamoja katika kukuza sekta ya utalii wa Zanzibar na kwa hapa Arusha," alisema.

Hata hivyo, alisema wamefika mkoani humo kuwaomba wadau katika sekta hiyo kujumuika nao kwenye tamasha hilo ambalo limelenga kuleta msukumo wa ukuaji wa kiuchumi kwenye eneo hilo.

Alisema kwa sasa uchumi wa Zanzibar kwa asilimia 30 unachangiwa na sekta ya utalii pamoja na asilimia 80 ya fedha za kigeni zinatokana na sekta hiyo.

Alisema mafanikio hayo yanatokana na kutanua wigo wa bidhaa zao za kitalii nje ya visiwa hivyo na mwaka 2022 walikuwa na watalii 550,000 na mwaka 2023 wameweza kuwa na watalii 638,449.

"Kwa uwekezaji tulioufanya ndani ya miaka mitatu kupitia chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, wamefanikiwa kuvutia jumla ya Sh. trilioni tano katika sekta ya utalii na kwa sekta nyingine wamevutia takribani Sh. trilioni 3.5," alisema.

Alisema katika maonesho hayo yatakuwa jukwaa la kimataifa litakalowakutanisha wawekezaji, watalii na wadau wa sekta mbalimbali za utalii kutoka ndani na nje ya nchi.

Vilevile, alisema maonesho yatawashirikisha wadau zaidi ya 250 wakiwamo wamiliki wa hoteli, vivutio vya utalii, kuendesha misafara ya kitalii na wawekezaji.

Alisema washiriki watapatiwa ujuzi na maarifa kwenye mafunzo kuhusu fursa za uwekezaji na maendeleo kupitia sekta hiyo.

Aidha, alisema kamisheni hiyo imeweka mpango mkakati wa kuendelea kutanua wigo kwenye sekta hiyo kwa kushirikiana na Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) na mikoa ya Tanzania Bara.

"Sehemu ambazo tunataka kutanua wigo ni pamoja na utalii wa urithi, utalii wa michezo na utalii wa afya ili kufikia malengo yao," aliongeza.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, alisema kazi waliyonayo ni kuhakikisha wanachochea na kutengeneza mazingira mazuri ya wafanyabiashara na wawekezaji ili wawalete wageni wengi ambao watachangia kupatikana kwa ajira kwa Watanzania.

"Ni ukweli usiopingika utalii ni moja ya nguzo kuu ya uchumi wetu pamoja na kuwa tuna vyanzo vingi, lakini kwenye mkoa hauwezi kuacha kuutambua utalii na kuupa nafasi yake kwa kuwa ni sehemu kubwa ambayo vijana wengi wamepata ajira," alisema.

Aliongeza: "Pia niwapongeze kwa kuja na mbinu hii ya kuwakusanya wadau kutoka sekta mbalimbali kwa kuwa na maonesho yatawapatia nafasi ya kujua Zanzibar wana vitu gani vizuri".

Katika hatua nyingine, Mkonda, aliwaagiza viongozi wanaosimamia vyama vya utalii kuhudhuria katika maonesho hayo kwa kuwa mambo watayojifunza yatawasaidia kufahamu namna ya kuongeza na kuwashawishi kwenda Arusha kutokana na bidhaa watakazoziona.

# Samia aagiza Kanisa Katoliki kurejeshewa eneo walilopokwa

**Na Godfrey Mushi,**
ARUSHA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amerejesha eneo la Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Arusha, ambalo lilitwaliwa na Halmashauri ya Jiji la Arusha.

Mbali ya kulirejesha, pia ameagiza Sh. milioni 500 zilizokuwa zimetolewa na kanisa hilo kwa ajili ya kununua tena eneo hilo warejeshewe.

Kwa mujibu wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, Rais Samia, ametumia mamlaka yake kikatiba kurejesha eneo hilo, baada ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, kuwasilisha ombi hilo la kanisa.

Mchengerwa alisema Rais Samia ameelekeza uongozi wa Mkoa wa Arusha na Halmashauri ya Jiji la Arusha, kurejesha eneo hilo kwa kanisa haraka pamoja na fedha hizo walizokuwa wametoa kwa ajili ya kununua eneo lao wenyewe.

> **"Na baadaye wakatakiwa kulilipia na fedha za michango zimetolewa shilingi milioni 500 ili kufidia eneo hilo na bahati nzuri eneo hili nimekuwa nikilifuatlia kwa karibu...**

"Nimekusikia Mkuu wa Mkoa (Makonda), umezungumza kwa hisia sana, umeeleza kwa masikitiko namna ambavyo eneo la Kanisa Katoliki walilolimiliki muda mrefu, likanyang'anywa sijui kwa utaratibu upi.

"Na baadaye wakatakiwa kulilipia na fedha za michango zimetolewa shilingi milioni 500 ili kufidia eneo hilo na bahati nzuri eneo hili nimekuwa nikilifuatlia kwa karibu, jana nilizungumza na Rais na kumweleza changamoto hii, akanipa haya maelekezo," alisema.

Aliongeza: "Rais amenielekeza eneo hilo lirejeshwe kwa kanisa mara moja na shilingi milioni 500 ambayo mliichukua kwa kanisa zirejeshwe na hili niwaelekeze mkoa kulisimamia kuhakikisha fedha hizi zinarudi kwa kanisa kama ambavyo namna mlivyozichukua kutoka kanisani".

Awali, Makonda alisema alikuta mgogoro huo na baada ya kukaa ndani walikuta mambo waliyodhani ndiyo kumbe siyo.

Alisema: "Fikiria licha ya eneo hilo kumilikiwa na kanisa awali ila nilikaa na Askofu akaniambia wameambiwa walipie na kupewa deadline na vitisho wakaamua kulipia kwa kutumia michango ya ujenzi na fedha ikakusanywa jimbo zima.

...Nilijisikia vibaya sana, nakuomba Waziri, ile ni sadaka tusile sadaka warudishiwe fedha na eneo lao."



Baadhi ya viongozi wa kimila wa jamii ya wafugaji (malaigwanani) wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, wakisikiliza maelekezo ya kuhamasisha jamii kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu kwenye kikao kilichofanyika mji mdogo wa Orkesumet juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Bil.44/- kutekeleza ujenzi Hospitali ya Manispaa

**Na Godfrey Mushi,**
MOSHI

SERIKALI imetenga zaidi ya Sh. bilioni 44 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Manispaa Moshi.

Uwekezaji wa vifaa tiba peke yake, utaigharimu serikali Sh. bilioni 44 na Sh. bilioni 1.8 ni za ujenzi, ambapo hadi kukamilika kwake itakuwa imegharimu Sh. bilioni sita.

Jana, Waziri wa Afya, Jenista Mhagama, alisema hayo baada ya kutembelea na kukagua ujenzi wa Hospitali ya Manispaa ya Moshi.

Waziri Mhagama alionyesha utofauti wa fedha zilizotolewa katika kipindi kilichopita na cha sasa; ili kuboresha miundombinu ya utolewaji wa huduma za afya nchini.

"Katika Mkoa wa Kilimanjaro kwa kipindi kilichopita ulipokea Sh.bilioni nane kwa ajili ya vifaa tiba, lakini kwa kipindi hiki kifupi, serikali imetoa shilingi bilioni 44 za ununuzi wa vifaa tiba ikiwamo X-Ray, Ct-Scan, vitanda vya wagonjwa, vitanda vya kujifungulia pamoja na dawa," alisema Waziri Mhagama.

Aidha, Waziri Mhagama akiwa katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Kata ya Mabogini, aliwaeleza wananchi kuwa serikali imeleta fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali, ikiwamo ya sekta ya afya.

Vilevile, alisema, Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, ikikamilika itakuwa na wodi za kulaza wagonjwa pamoja na nyumba za watumishi, ili wananchi wasipate tabu pindi wanapotaka kupata huduma za afya.



# Mgodi kuongeza idadi ya wanawake hadi 50%

**Na Faustine Feliciane, aliyekuwa** SHINYANGA

UONGOZI wa migodi ya kuchimba dhahabu ya Barrick North Mara mkoani Mara na Bulyanhulu ulioko Kahama mkoani Shinyanga, umesema upo kwenye mpango wa kuongeza idadi ya wafanyakazi wanawake kutoka asilimia 11 mpaka 50.

Rais na Mtendaji Mkuu wa Barrick, Mark Bristow, alisema hayo juzi mkoani hapa kwenye mkutano wa robo ya nne ya mwaka uliowakutanisha uongozi wa Barrick, serikali wawakilishi wa wananchi na wadau wengine.

Alisema migodi hiyo inatoa nafasi kwa wanawake kufanya kazi ambapo mpaka sasa wamefikia asilimia 11 ya wafanyakazi wote lakini wanataka wafike asilimia 50.

Bristow alisema wanawake wamekuwa wakifanya vizuri zaidi kwenye migodi hiyo wakiwa na uwezo mkubwa wa kuendesha mitambo mbalimbali.

Aidha, alisema wanatamani kufikia lengo hilo kutokana na kushawishika na juhudi za serikali ya kutoa nafasi nyingi kwa wanawake kwenye nafasi mbalimbali za uongozi.

"Serikali ya Tanzania ni mfano mkubwa na mzuri kwa mataifa mengine kwa kutoa nafasi kubwa kwa wanawake kwenye uongozi katika sekta mbalimbali, na sisi Barrick tunataka kuunga mkono kwa kutoa nafasi kwa wanawake," alisema Bristow.

Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano wa Kampuni hiyo, Georgia Mutagahywa, alisema wameanza kuwafuatilia wanafunzi wanawake wakiwa shuleni na kuwahamasisha wasome masuala ya uchimbaji madini.

Alisema: "Lakini pia wanafunzi hawa tunawatembelea shuleni, tunawaalika migodini kuangalia namna shughuli zinavyoendeshwa, tumekuwa tukiwahamasisha sana kusoma masuala ya madini wajikite huko kupata elimu na nafasi ya kufanya kazi migodini".

# Waziri ashangaa chenji kubaki ujenzi wa madarasa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Ndejembi, ameshangaa hatua ya Kamati ya Shule ya Sekondari Ntobo iliyoko Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga kubakiza Sh. milioni 11 kati ya Sh. milioni 182 walizopewa kwa ajili ya kujenga mradi wa vyumba saba vya madarasa.

Mradi wa ujenzi wa vyumba hivyo umegharimu Sh. milioni 170, ukihusisha pia matundu manane ya vyoo vya wanafunzi pamoja na ofisi moja ya walimu.

Akizungumza baada ya kukagua miradi hiyo jana, Ndejembi aliipongeza kamati hiyo akisema miradi mingi utekelezaji wake unakuwa na upungufu wa fedha ikiwamo kuisha kabla ya mradi kukamilika au mradi ukikamilika unakuwa chini ya viwango.

Alisema, serikali imekuwa ikitekeleza miradi ya maendeleo kwa awamu kulingana na inavyopata fedha na madarasa hayo yatasaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani.

Alisema wanafunzi watasoma na kutimiza ndoto zao kwa kuwa mazingira rafiki ya kujisomea wameshayatengeneza kwa kuwa na vyumba vya madarasa safi.

Awali akitoa taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo, Mwalimu Mkuu wa Sekondari ya Ntobo, Hussein Mbwambo, alisema walipokea Sh. milioni 182 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa saba ya wanafunzi na zikatumika Sh.milioni 170.892 na kubaki Sh.11.107.

Alisema katika kujenga ofisi moja ya walimu pia wameweza kubakiza chenji na wamemwandikia barua Mkurugenzi wa Halmashauri ili kuwapatia idhini ya kutumia Sh.milioni 15 ili kurekebisha jengo la utawala kuwa la kisasa.

Mbwambo alisema matundu ya vyoo yameweka uwiano kwa wanafunzi kulinganisha na ilivyokuwa awali na madarasa yameweka mazingira wezeshi ya kujifunzia kwa kuwa na viti na meza.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, akikagua ujenzi wa choo cha wasichana katika Shule ya Sekondari Masekelo, Manispaa ya Shinyanga, chenye matundu 12 pamoja na chumba maalumu cha kujistiri hedhi, kilichojengwa na Taasisi ya Flaviana Matata kwa ufadhili wa Diamond Do Good, mwishoni mwa wiki. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Wanaotumia sherehe kukeketa mabinti waonywa

**Na Waandishi Wetu**

JESHI la Polisi Kanda Maalumu ya Tarime/Rorya limewaonya wazazi na mangariba wilayani Tarime mkoani Mara wanaojiandaa kufanya sherehe za tohara kila mwishoni mwa mwaka kutokufanya hivyo, kwani watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Kamanda wa jeshi hilo, ACP Mark Njera alitoa onyo hilo na kuahidi kuwachukulia hatua kali za kisheria jamii zote zitakazohusika.

Kamanda Njera alisema jeshi hilo litachukua hatua kali kwa wale wote watakaobainika kushiriki katika vitendo vya ukeketaji dhidi ya watoto wa kike.

Njera alitoa kauli hiyo juzi katika Mji wa Nyamongo wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wasichana zaidi ya 200 yaliyolenga kupinga ukatili wa kijinsia wanaotarajiwa kujiunga kidato cha kwanza, tano na vyuo mwakani.

Alisema tayari jeshi hilo lina taarifa juu ya baadhi ya koo zaidi ya tisa wilayani hapa kuanza maandalizi ya mapema kushiriki katika vitendo vya ukeketaji ikiwa ni pamoja na kuwaondoa shuleni wasichana wadogo.

Kwa mujibu wa Mratibu wa Kitengo cha Dawati la Jinsia katika mkoa huo wa kipolisi, Claude Mtweve baadhi ya jamii hizo huwarubuni wasichana hao kwa kuwapatia zawadi mbalimbali kama vile fedha na nguo ili kuwashawishi kushiriki ukeketaji.

**Baadhi ya washiriki akiwamo, Agnes Marwa alikiri kuwa mila hizo zimepitwa na wakati na kuwa wapo tayari kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi pamoja na wadau wengine ....**

Mafunzo hayo ambayo yalikuwa na kauli mbiu "Tuambiwe kabla hawajaharibiwa" yalilenga pia kuwawezesha wasichana wadogo kuunda vikundi vya mawasiliano shuleni kwa lengo la kukusanya taarifa za ukatili wa kijinsia maeneo yao.

Baadhi ya washiriki akiwamo, Agnes Marwa alikiri kuwa mila hizo zimepitwa na wakati na kuwa wapo tayari kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi pamoja na wadau wengine kuhakikisha wanazima majaribio yote ya namna hiyo.

Aidha, walieleza kuwa koo hizo wamekuwa wakitumia mbinu mbalimbali kukwepa mkono wa sheria ikiwa ni pamoja na kuwavusha nchi jirani ambapo pia kuna koo na makabila yanayofanana pande zote.

"Mbinu nyingine ni pamoja na kuwavalisha wasichana nguo za kiume sanjari na kuwakeketa nyakati za usiku, huku kukiwa na ulinzi wa vijana wa jadi hatua ambayo inakuwa vigumu kuwabaini," alisema mshiriki ambaye hata hivyo hakupenda kuandikwa jina gazetini.

Mwaka 1997, Shirika la Afya Duniani (WHO) ilitoa tamko la pamoja dhidi ya mila ya ukeketaji kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA).

Kila baada ya miaka miwili baadhi ya koo za jamii wilayani hapa hutekeleza utamaduni wa kufanya tohara kwa vijana wa kiume, huku kukiwa na madai pia ya kufanyiwa ukeketaji watoto wa wadogo wa kike.

**Imeandaliwa na Ambrose Wantaigwa, Samson Chacha (TARIME)**



Ukurasa 12

**SIMU NI JASUSI**
**Unayeitumia hufichi kitu unabeba bomu mfukoni**



Ukurasa 13

Madaktari wanawake waja kimkakati kukabili unyanyasaji kijinsia, afya akili



Ukurasa 14

**Misitu vijijini ilivyo kisima cha utajiri kwa wananchi**

Nipashe TESA

Jumanne Oktoba 8, 2024

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

ELIMU

NA CHRISTINA MWAKANGALE

SHIDA AFYA YA AKILI KWA WATOTO

# Mbumbumbu darasani, viburi, utundu sana, kuvunja vyombo vyote ni viashiria, fuatilieni

DUNIA imebadilika mzazi au mlezi, akumbuke kufuatilia watoto wa chini ya miaka saba, umri wa kuanza darasa la kwanza kubaini iwapo wana changamoto za afya ya akili.

Baadhi ya mambo unayoweza kuyapima kubaina kama ana matatizo ni pamoja na kutowaogopa wageni. Anawarukia, kuwazoea ghafla hata wakati mwingine kuwapokonya chakula au kinywaji wanapokaribishwa.

Akiambiwa afanye kazi kama kuondoa sahani mezani baada ya kula anakasirika, kuitupa chini, anapasua vyombo, hana utii wala woga anafanya anachotaka.

Watoto wenzake wanamtenga hawachezi naye, anawapiga na kuharibu vitu vyao. Licha ya kusoma shule za awali tangu miaka mitatu hawezi kusoma, kutamka herufi na kutambua picha.

Kwa ujumla afya ya akili inahusiana moja kwa moja na kile mtu anachokiishi leo na kufunzwa utotoni katika umri wa 'chekechea' au shule ya awali.

Mtaalamu wa Saikoloji na Mhadhiri wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE) Dk. Nabwera Rashid, amefanya utafiti na kubaini kasoro za uelewa kwa watoto na shida ya afya ya akili.

Akiwasilisha matokeo ya utafiti uliohusu: afya ya akili ya watoto wa shule ya awali na uhusiano kwenye matokeo ya masomo ya awali nchini, anasema makuzi ya watoto kuanzia tumboni mwa mama hadi umri wa shule ya awali ni muhimu mno.



Malezi na makuzi ya mtoto yanahusika moja kwa moja na afya ya akili. **PICHA MTANDAO**

Anazungumzia utafiti huo, kwenye mkutano ulioandaliwa na Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wadau wa Afya ya Akili Tanzania (TMH-CoP) ECHO, akisema afya timamu ya akili utotoni inahusisha ustawi wa kihisia, kijamii na kisaikolojia.

Akifafanua zaidi, anasema ni kwa watoto wenye umri sifuri hadi miaka mitano.

Utafiti alioufanya ulihusisha shule 12 kutoka wilaya tatu za Arumeru mkoani Arusha, Kinondoni Dar es Salaam na Nzega Tabora, ukishirikisha watoto 403 wa miaka ziro hadi saba, kati yao wasichana wakiwa ni asilimia 49.6.

"Mara nyingi mijadala kama hii ya afya ya akili huhusisha vijana sasa huu umelenga watoto nao wanaathiriwa na tatizo la akili. Asilimia 40 ya watoto wanaoishi Afrika, ni kati ya idadi yote ya watu duniani. Wasipolelewa ipasavyo, kuna athari nao ni wazazi wajao."

Anasema mtoto anakumbwa na changamoto za kiafya kama tatizo la akili na katika umri huo, hujaribu kukabiliana na hisia zake na masuala mengine ya kijamii.

Na huu ndiyo umri wa kuanza shule kwa mujibu wa sera ya elimu ya Tanzania na pia ni kipindi cha kumtengeneza mtoto amudu kuishi katika jamii. Wengi wa umri huu wanaingia elimu ya awali, wanafundishwa mambo mengi.

Mfano kusalimia, kuwa na marafiki, kunawa mikono na kusema asante au samahani na asipopata elimu atakutana na watu ukubwani, akiwa hana hisia zozote iwe shukrani au huzuni.

Ananukuu Shirika la Afya Duniani (WHO) kuwa, kwenye kila watoto 10 unaokutana nao njiani watatu hadi watano wana tatizo la akili.

Utafiti wake, anasema umebaini kuwa kati ya watoto 403 waliotafitiwa, baadhi wakiwa madarasa ya awali kwa madaraja tofauti, 169 sawa na asilimia 41, hawako sawa katika afya ya akili na kuathiri ujifunzaji.

Dk. Nabwera, anataja maeneo ambayo watoto hao huathirika zaidi ni kuelewa hatua za kusoma kama vile kufahamu 'fonimu' mfano K, U na D.

Hawawezi kutaja majina ya picha, ujuzi wa msamiati na fonetiki ambayo ni matamshi ya maneno humtatiza pia.

"Watoto watundu wanaosababisha matatizo kadhaa ni 131 kati ya waliohusishwa kwenye utafiti huu. Nilibaini watoto ni watundu sana yaani hawatulii hata kidogo na darasani pia," anasema.

Anafafanua kuwa Dar es Salaam Kinondoni alikofanyia utafiti ni miongoni mwa mikoa ambayo wazazi na walezi wana shughuli nyingi na hawana muda wa kulea hawa watoto.

Anafafanua kuwa katika kila watoto 10 unaokutana nao njiani watatu hadi watano, wana tatizo la akili.

Matokeo yanaonesha kuwa asilimia 58 ambao ni sawa na watoto 235 wa shule ya awali, walikuwa na alama chini ya wastani katika mtihani wa ujuzi wa kusoma Kiswahili.

Mhadhiri huyo anasema inamaanisha wengi wa watoto wa shule ya awali hawakuwa na ujuzi wa kutaja alfabeti mfano A,B,C,D,E, F...., sauti za alfabeti, kusoma na kuelewa, kushika na kufungua vitabu, utambulisho wa barua na majina ya picha.

Anasema umri huo ndiyo wa kuanza shule, akisisitiza haja ya watoto wa umri huo, kufuatiliwa uwezo wa uelewa kwasababu nao huathirika na afya ya akili.

"Watoto wengi umri huu, ndio wanaingia elimu ya awali, wanafundishwa kusalimia, kuwa na marafiki, kunawa mikono na kusema asante, au samahani na wasipopata elimu hiyo itakuwa tatizo ukubwani ...."

**INAENDELEA UK.12**

TEKNOLOJIA

NA MWANDISHI WETU

SIMU NI JASUSI

# Unayeitumia hufichi kitu unabeba bomu mfukoni

UJASUSI wa kidijitali ni jambo linalowahusu wanaotumia vifaa vya mawasiliano kama simu janja au 'smartphones' kuujua ukweli kwamba wanatembea na bomu linalolipuka mfukoni.

Ni kama kubeba mzinga wa nyuki wanaoweza kukung'ata na kukuangamiza. Kwa sababu majasusi wanadukua taarifa zako wanavyotaka bila wewe uliyeiweka mfukoni au kwenye pochi kujijua.


Wanaweza kutizama maandiko (text), ujumbe (SMS), picha na kutumia kamera kukupata mubashara kwenye video au vyovyote wanavyohitaji.

Kwa hiyo simu ya mkononi ni jasusi usiyelijua lakini uliyembeba. "Watu wanaonekana hawaelewi kwamba usalama wa simu za mkononi kama kitu kimoja ni jambo ambalo halipo," inasema BBC.

Inaeleza wasiwasi mkubwa kwamba hakuna faragha kwenye simu za mkononi kwa sababu zimebainika kuwa na programu za kijasusi. Mojawapo ni kama 'Pegasus', inayotengenezwa na kampuni ya NSO Group ya Israel.

Programu ya ujasusi ya Pegasus kutoka kampuni ya NSO Group ilizua maswali kuhusu usalama wa simu janja.

Miaka ya karibuni imegundulika kuwa programu ya Pegasus inaweza kukuweka kwenye simu za iPhones na Android, na kuruhusu kutoa ujumbe, picha na barua pepe, kurekodi simu na kuwasha kipaza sauti au 'mic' na kamera na kufanya kazi yake kwa siri kama majasusi wanavyotaka na kuiongoza.



Simu inakudukua, chunga. **PICHA: MTANDAO**

Kiasi teknolojia inavyoendelea haraka na kwa nguvu upelelezi na uchunguzi sasa hivi unawafanya wanaotumia simu 'kuonekana mno' au kuachwa wazi bila kificho ama kizuizi cha kudukuliwa.

Uchunguzi wa Kituo cha Utafiti cha Pew unaonyesha kuwa Wamarekani asilimia 72 waliripoti kuwa wanachunguzwa katika simu zao na kufuatiliwa.

Wanaowadukua ni watangazaji wa matangazo ya biashara, kampuni za teknolojia au kampuni zingine na idadi kubwa inaamini kuwa shughuli zao nyingi mtandaoni zinafuatiliwa na serikali.

Ni wazi kuwa kuna uingiliaji wa aina nyingine na kwamba hakuna ulinzi kwenye masuala ya kutumia simu janja. Ni kama kutembea bila mavazi.

Japo si kila mtu lakini wapo baadhi ambao majasusi wanawafanyia kazi kwa niaba ya serikali zao, kampuni au hata usalama wa mataifa.

Dunia leo inathibitika kuwa matumizi ya simu za mkononi yanakuja na madhara ambayo mwanzoni watu wengi hawakuyajua kuwa yanaweza kuvuruga maisha yao.

Sio tu kiafya bali pia kisaikolojia na hata kuyahatarisha maana vilipuzi vinaweza kutumiwa kwa njia ya simu na kukuangamiza.

Simu ina alama za vidole, ina picha, anuani, umri, uraia na popote unapoishika unaonekana.

Baadhi ya matukio ya kutumia ujasusi wa vifaa vya kielektroniki zikiwamo simu za mkononi na kuua watu ni lile la kushambuliwa kiongozi wa kundi la Hezbollah la Lebanon Hassan Nasrallah.

Pamoja naye, udukuzi wa kupitia vifaa vya kielektroniki umeharibu vifaa vya mawasiliano kuanzia simu za upepo, za mkononi, kompyuta na vifaa vingine vyote vya kundi la Hezbollah.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine (SAUT) Mwanza, Dk. Kamugisha Byabato, anasema matumizi ya ujasusi kwenye vifaa vya kielektroniki yanaakisi ukweli kuwa watumiaji wa simu hizo wameanikwa zaidi.

Anakumbusha kuwa hakuna kificho cha mahali ulipo, unachofanya na kwa ujumla shughuli zako zama hizi.

Mtaalamu wa uhandisi wa nishati mbadala na teknolojia anasema ni jambo ambalo linaamsha wataalamu kubuni na kuanzisha njia nyingine zenye usalama zaidi za mawasiliano.

Anaeleza kuwa zinahitajika juhudi nyingine zaidi ya kuibua na kutumia mawasiliano hayo iwapo taifa linahitaji kuwa na usalama zaidi.

Anasema japo si kila mtu anaweza kudukuliwa wala kufuatiliwa lakini, ukweli ni kwamba hakuna kificho kwenye simu janja.

Na majasusi wanafahamu wanaowalenga pote duniani hivyo tahadhari ni muhimu.

Anaeleza kuwa dunia ya sasa ujasusi unaweza kutumia simu hizo na vifaa vya kielektroniki kupata chochote wanachotaka.

Anaongeza kuwa wanaweza kufuatilia mwenendo wa watu wanaowaona kuwa ni hatari au wanaotishia maslahi yao, popote duniani.

Kwa mfano kupitia simu na vifaa vya mawasiliano vya kielektroniki mfano GPS, majasusi au yeyote anayehitaji taarifa za mtu fulani anavitumia kumfikia na kupata kile anachokitaka.

## Mbumbumbu darasani, viburi, utundu, kuvunja vyombo vyote ni viashiria

**INATOKA UK.11**

Anasema asilimia 2.8 ya watoto wa umri huo katika utafiti aliufanya, wapo darasani kwa madaraja tofauti kuanzia shule za awali na katika kila darasa moja watoto watano hadi 10 wana tatizo la akili.

Anataja uchokozi, wizi, uongo, hasira hadi wanaojipiga chini kuwa nyuma yake kuna tatizo la akili na mzazi au mlezi ama jamii haijatambua.

Anakumbusha kuwa labda wakiwa darasani wanaambiwa nenda mbele kasome au nenda kulala hatekelezi maagizo, fahamu kuna shida.

Anaeleza kuwa mtoto anapomaliza kula anatupa sahani chini na kuivunja au haipeleki inapotakiwa hilo ni tatizo na kwamba anayefanya vizuri ameshaanza kujua kuwa huyu ni mtu mzima na huyu ni mdogo.

Mhadhiri huyo anasema mtoto aliye na afya duni ya akili akiwa chini ya miaka mitano, akifikia miaka 14 tatizo litaongezeka.

Anasema elimu ya afya kwa watoto hao ni muhimu kutokana na kujumuisha theluthi moja ya watu wote duniani na asilimia 40 kati yao wanaishi Afrika, kwa mujibu wa Mifuko ya Idadi ya Watu wa Umoja wa Mataifa.

Anasema asilimia 2.8 ya Tanzania miaka mitatu hadi sita wanahudhuria shule ya awali akinukuu ripoti ya UNICEF, 2020.

Takwimu za hivi karibuni kimataifa, zinaonyesha katika nchi za Kusini Jangwa la Sahara, takribani watoto milioni 202 wenye miaka kati ya minne hadi 14 hawawezi kusoma kwa ustadi baada ya kuhitimu.

Dk. Nabwera, anasema umri wa miaka mitatu hadi sita, mtoto anaanza kuonyesha hisia zake, mfano ukimwambia kitu hajibu wala hafanyi bali anatoa machozi.

Anaeleza kuwa mtoto akiwa darasani unamwambia nenda mbele kasome au kalale hatekelezi fahamu kuna shida.

Anamtaja mtoto anayempiga mwenzake na aliyepigwa asimrudishie fahamu, aliyempiga hawezi kumudu hisia zake lakini ambaye hakumrudishia anazimudu hisia zake.

Watoto wanatakiwa kufanya kanuni za darasani au nyumbani, watoto wengine utakuta amekaa dawati hili ameshafika nyuma, au keshatoka nje. Muda wa kula anataka kuimba, wa kuoga e anataka kula, hii ni dalili ya mtoto ameshindwa kumudu hisia zake na majukumu kijamii.

Anasema utafiti hutumia maswali kuuliza watoto kubaini wana tabia mbaya au nzuri, mfano mwalimu anamwambia usifanye hiki anafanya, au mzazi anamkataza usiende nyumba fulani kuna hiki au mtoto anang'oa maua au ukoka uliopandwa.

Anataja tatizo la aibu, ukimwambia nenda mbele analia, mwalimu akimpa kazi anasema anaumwa tumbo.

Anazungumzia mtoto kushindwa kutengeneza marafiki, usimhukumu chunguza kuna tabia ambazo anazo na wen,ake hawazikubali, akiwa nao anawapiga, anahatibu vitu vya wenzake.

ELIMU
NA MWANDISHI WETU

# Madaktari wanawake waja kimkakati kukabili unyanyasaji kijinsia, afya akili

**• Ni MEWATA yaanzisha rasmi tawi Zanzibar**

TANZANIA Bara hadi Visiwani, ukatili wa kijinsia kwa jinsi zote ni janga, serikali na wadau wanashirikiana kukabiliana na balaa hilo la mmomonyoko wa maadili linalowaumiza zaidi watoto wa kike, wakiume na wanawake wakiwamo vikongwe.

Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania (MEWATA), ni miongoni mwa mashiriki yanayopambana na ukatili huo, na hivi karibuni Dk. Zeitun Bokhary, rais wa MEWATA, anakiri kuwa jinsi zote zinaathirika na lazima kuchukua hatua na kusimama pamoja kuwalinda dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia.

Ni katika mahojiano na Nipashe jijini Dar es Salaam, anapoeleza kuwa unyanyasaji unaumiza wote na MEWATA inaliona kuwa ni tatizo la kitaifa na imeanza kutoa elimu kwa umma ili watambua kuwa wamiliki na wenye mamlaka ya miili na maisha yao. Kama anavyosimulia zaidi...

**SWALI: Mnachukua hatua gani tofauti na juhudi nyingi zinazofanyika?**

**JIBU:** Tunafika shuleni kuwafundisha wanafunzi wajitambue kuwa miili yao zikiwamo sehemu za siri ni mali yao hakuna yeyote anayeruhusiwa kuwagusa au kuziona.

Wanatakiwa kufahamu hayo kwa kuwa ndiyo mwanzo wa kuwanyanyasa. Mathalani, tunawaeleza umuhimu wa viungo hivyo, pamoja na matumizi ya miili yao mfano sehemu za siri na matiti. Tunawaambia ni wakati upi vitatumika, siyo sasa wakiwa watoto. Tunawaelimisha kuwa miili yao si ya kuchezewa na mtu mwingine na wasiruhusu, walipinge na kutoa taarifa za wanyanyasaji.

Tunawafundisha kuhusu kudanganywa na watu wanaowahadaa kutumia simu na kuwarekodi na kuwapiga picha zinazosambazwa mitandaoni. Kingine ni aina za unyanyasaji kama kulazimishiwa kuolewa, kutumikishwa kwenye ajira.

Pamoja na kuelimisha hatari za ukatili wa kijinsia, tunawekeza pia kwenye kutoa elimu ya kufahamu na kutibu matatizo ya afya ya akili kwa watoto. Tumegundua kuwa linaathiri maendeleo darasani na ndani ya jamii.

Kadhalika, tunawahamasisha mabinti kusoma masomo ya sayansi ili kuwa na idadi kubwa ya wataalamu wanawake kwenye sayansi na kiteknolojia, kuanzia madaktari, wahandisi, mabingwa wa upasuaji, marubani na manahodha.



Dk. Zeitun Bokhary (wa pili kushoto) pamoja na mwasisi wa MEWATA, Prof. Ester Mwaikambo (kushoto) na madaktari wengine, wakati wa Mkutano Mkuu wa Kitaifa wa Afya, uliomalizika Zanzibar. **PICHA: MEWATA**

Tunahamasisha hivyo ili kuondoa pengo la jinsia kwenye sekta ya sayansi na teknolojia kwa kuongeza wanawake kwenye kazi ambazo zinaaminika kuwa hawaziwezi.

**SWALI: Maono ya MEWATA ni kuwa na Watanzania wenye afya bora wanaopata huduma bora, nafuu na endelevu kupitia mifumo bora inayoamini. Juhudi hizo zimefikia wapi?**

**JIBU:** Harakati za chama tangu kilipoanzishwa ni kuwa na jamii yenye afya bora na kuhudumiwa kwa ubora.

Itakumbukwa kuwa miongoni mwa wataalamu wa afya walioasisi kampeni za kuelimisha jamii kutambua na kutibu saratani ya matiti na shingo ya kizazi ni sisi chama cha madaktari wanawake na sasa juhudi zinaendelea.

Tangu mwanzo kampeni na hamasa zimefanyika na kuwafikia wanawake karibu Tanzania nzima kuelezea kuzitambua dalili na kutibu magonjwa ya saratani ya matiti na shingo ya kizazi.

Wanawake wengi wanajitokeza wanafuatilia afya ya matiti na shingo ya kizazi. Itakumbukwa kwamba kwa kufanya uchunguzi (screening), kinamama wengi wenye dalili waligundulika na kutibiwa.

Licha ya kwamba walikuwa wana dalili hawakuzifahamu lakini kampeni na uchunguzi wa MEWATA ulifanikisha kuwatambua, kutibiwa mapema na kupona.

Kampeni zinaendelea na kukumbusha kuwa saratani ikigundulika mapema inatibika na kuwashauri kujichunguza, kushiriki kampeni kila zinapotangazwa na kuwahi hospitalini.

Tunawakumbusha kuwa Oktoba ni mwezi wa kuhamasisha uelewa, kuchukua hatua na kutiba saratani ya matiti, nasi tutaendelea na jukumu hilo.

Watanzania wafahamu kuwa changamoto kubwa ya saratani ni kuchelewa kuigundua na kuanza tiba mapema.

Pamoja na kuwaeleza na kuwachunguza saratani za matiti na shingo ya kizazi tunawafahamisha kuhusu mambo yanayochangia kupata maradhi hayo kama kutumia tumbaku, vilevi, dawa za kulevya ili kujiepusha.

**SWALI: Tueleze kuhusu harakati za MEWATA Zanzibar.**

**JIBU:** Kwa karibu miongo mitatu kazi za MEWATA zilifanyika zaidi Bara, lakini mwaka huu tumeanzisha tawi Zanzibar.

Tumefungua tawi Zanzibar wiki iliyopita tukiwa na wanachama zaidi ya 20 ambao ni pamoja na mabingwa wa watoto, wanawake, wapasuaji na kwa ujumla MEWATA sasa iko Bara na Visiwani.

> Tunaishauri jamii kusoma taarifa mbalimbali za kiafya aidha majarida, magazeti, vipeperushi vya kiafya na pia mabango na ujumbe unaoweka kwenye huduma za afya.

Kwa mara ya kwanza tumepokea wanachama wapya madaktari wanawake Zanzibar, ni tukio la kihistoria MEWATA mwaka 2024 imeandika rekodi, tutashirikiana nao kwenye kufikia maono yetu.

Ni matokeo ya Mkutano Mkuu wa Afya (Tanzania Healthy Summit) uliofanyika karibuni.

**SWALI: Unazungumziaje wanachama na idadi ya madaktari wanawake kitaifa sasa?**

**JIBU:** Kwa ujumla idadi ya wanachama inaongezeka kama madaktari wanavyoongezeka pia, tupo takribani wana MEWATA 500 wakiwamo wanachama hai wanaolipa michango na ada za chama, tunafikia 250. Lakini tunao wengine wasio hai.

Idadi ya wanawake madaktari pia inaongezeka ikilinganishwa na ilivyokuwa hapo awali. Wasichana wanasoma sayansi na wanaoingia kwenye fani ya tiba siyo kama zamani miaka ya 1990 wanazidi kuongezeka.

**SWALI: Ni nini ujumbe wako kwa jamii na serikali?**

**JIBU:** Kinamama tujali afya ya uzazi na uzazi salama. Tanzania imepunguza idadi ya vifo vya wazazi kutoka 500 kwa kila vizazi hai 100,000 hadi kufikia wastani wa vifo 100.

Tunawahimiza wajawazito kuhudhuria kliniki na kupata matibabu, ushauri, maelekezo na mafundisho na kuyafuata.

Wajawazito wasijifungulie nyumbani, wafike kwenye vituo vya afya kupata matibabu, kwa kufanya hivyo itapunguza vifo vya wajawazito, na watoto wachanga.

Tunaishauri jamii kusoma taarifa mbalimbali za kiafya aidha majarida, magazeti, vipeperushi vya kiafya na pia mabango na ujumbe unaoweka kwenye huduma za afya.

Watu wazingatie lishe bora, afya ya akili, tiba, chanjo magonjwa ya milipuko na kutafuta tiba sahihi, ikumbukwe afya ni mtaji wa kwanza kwenye kila kitu.

Kadhalika sekta ya afya imekuwa na mafanikio makubwa, serikali imejenga miundombinu bora vijijini na sehemu nyingi hata za vitongoji vya ndani zaidi, leo zina huduma za afya karibu na wananchi.

Tunampongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuboresha afya ya wananchi na serikali bado inaendelea.

ELIMU

NA CHRISTINA HAULE, MOROGORO

# Misitu vijijini ilivyo kisima cha utajiri kwa wananchi

KUWAPO kwa misitu ya vijiji katika mikoa mbalimbali ni fursa ya kufuga nyuki kibiashara pamoja na kutunza mazingira na kukabili athari za mabadiliko ya tabianchi.

Ni ujumbe unaoelekezwa kwa wanachama wa Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA), walio kwenye kanda sita za kitaifa.

Wanashauriwa kuanzisha miradi ya ufugaji nyuki katika misitu ya vijiji, kuitunza na kuongeza mapato sambamba na kuhifadhi mazingira.

Meneja Mradi wa Forest and Farm Facility (FFF) wa MJUMITA Daniel Lucas, anasema hayo kwenye mkutano mkuu wa wanachama wa mtandao huo ukileta pamoja wajumbe 1,500 wa kanda hizo sita.

Wajumbe hao ni pamoja na maofisa misitu, madiwani, viongozi wa vijiji, wafadhili na wafanyakazi wa Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG).

Anasema kufuga nyuki kibiashara ni muhimu kwani kunalinda mazingira kwa sababu huzingatia kanuni za kitaalamu na kutunza ikolojia.

Anaongeza kuwa kuna misitu mingi ya asili inayofaa kuzalisha asali na wananchi wakijikita katika miradi ya nyuki watakuwa wasimamizi misitu kwa ufanisi zaidi.

"Kama tutafuga nyuki na kushiriki kikamilifu kuhifadhi misitu na kuongeza kipato kupitia uzalishaji wa asali na bidhaa nyingine zitokanazo na nyuki tutaboresha maisha," anasema.

"Tutazalisha asali, nta ya nyuki, sumu ya nyuki, chavua, sabuni na kupata vipodozi vya ngozi na nywele na manukato hatimaye kujiongezea kipato na kuhifadhi misitu. Ndiko kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi." Anasema Lucas.

Akielezea mchango wa MJUMITA kwa jamii kupitia sekta ya kufuga nyuki, Lucas anasema wametoa mafunzo ya namna ya kuongeza thamani kwenye mazao ya nyuki kwa watu 61 ambao kati yao wanawake ni 48 na wanaume 13.

Aidha, mtandao umeunganisha wafuga nyuki na kuanzisha shirikisho wilayani Kilosa, kuandaa kitabu cha ufugaji nyuki kwa ajili wanafunzi wa shule za msingi kujifunzia ili washiriki kwenye kuhifadhi misitu.

Kadhalika, anataja kupata wanachama wa MJUMITA ambao wanaanzia ngazi ya chini hadi kufikia viwango vya juu vya ukuaji.



Kufuga nyuki moja ya shughuli zinazofanyika vijijini. **PICHA: MTANDAO**

> "Kama tutafuga nyuki na kushiriki kikamilifu kuhifadhi misitu na kuongeza kipato kupitia uzalishaji wa asali na bidhaa nyingine zitokanazo na nyuki tutaboresha maisha.



Aidha, Lucas anasema MJUMITA imeshindanisha shule za msingi kupitia uandishi wa insha na kutoa mizinga 100 kwa shule 10 zilizoshiriki mashindano sambamba na kushiriki maonyesho ya kikanda na kitaifa.

Lengo ni kufikia masoko na kutangaza bidhaa zinazotokana asali na kuanzisha manzuki ya mfano kwa ajili ya ufugaji nyuki.

### TANZANIA IKO JUU

Tanzania ni ya pili kwa kuzalisha asali barani Afrika baada ya Ethiopia na inashika nafasi ya 14 duniani.

Mwaka 2022, ilizalisha tani 32,691 za asali na kwa sasa inachangia asilimia 1.7 ya asali yote inayozalishwa duniani.

Lucas anasema sekta hiyo huchangia Dola za Marekani milioni 5.8 kwa mwaka kazi ikifanywa na jamii zinazoishi pembezoni mwa misitu kama shughuli za kijadi.

### KUFUGA KIZAMANI

Kadhalika, asilimia 90 ya ufugaji nyuki hufanywa kwa njia ya kienyeji na asilimia 70 ni mizinga ya asili.

Ufugaji kienyeji unafanywa na makabila mengi kimazoea kwa kutumia mizinga ya asili bila kuzingatia kanuni bora za ufugaji. Matokeo yake ni kuambulia mazao kiduchu kutokana na matumizi ya zana za asili, duni na kuwaacha nyuki kuzagaa pasipo uangalizi wa karibu.

Uwekezaji huo ni hasara ndiyo maana kuwekeza kwenye ufugaji wa tija au kibiashara kwa kutumia mbinu na kanuni bora kama kutumia mizinga ya masanduku yenye viunzi au fremu na iliyo na kitenga malkia. Kadhalika unavuna mazao mengi kama asali, nta, maziwa na sumu ni muhimu.

Anasisitiza kuwa sekta ya ufugaji nyuki ina uwezo mkubwa wa kuongeza uchumi wa taifa, kuboresha maisha, kutoa ajira, kuongeza kipato na kutatua matatizo ya kiafya, kuhakikisha usalama wa chakula, na kudumisha mifumo ya ikolojia kupitia uchavushaji mimea.

Washiriki wa mkutano huo akiwamo Baraka Ibrahimu wanaiomba serikali kuweka utaratibu wa kuwapimia misitu ya hifadhi ya vijiji iliyoko karibu na wananchi na kuwapatia hati miliki ambazo zitawawezesha kuwa na uhalali wa kuendesha shughuli mbalimbali kama ulinzi, uhifadhi na kufugaji nyuki.

Aidha, anasema wanawaomba viongozi wa vijiji na madiwani kusimamia sheria za matumizi bora ya ardhi ili kuepukana na changamoto za migogoro ya ardhi ambayo inasababisha kuleta uvunjifu wa amani na hivyo nchi kuwa salama.

Anaiomba MJUMITA kutoa elimu zaidi kwa wananchi kuhusu sheria za ardhi na uhifadhi wa misitu na mazingira kwa sababu wengi hasa vijijini hawafahamu sheria hizo ambazo zinapunguza migogoro ya ardhi.

"Usimamizi wa misitu na ufugaji nyuki unapaswa kufuatwa kisheria na ikiwa mtu atahitaji kufanya ufugaji nyuki anapaswa kuzijua sheria za uhifadhi wa mazingira kwasababu ni sehemu ya uhifadhi, usimamizi na utunzaji wa mazingira," anasema.

Mkurugenzi Mtendaji wa MJUMITA, Rahima Njaidi, anasema wamejadiliana na wadau pamoja na serikali kuangalia changamoto wanazokutana nazo katika uhifadhi na usimamizi wa misitu.

Aidha, kupanga mkakati wa kupunguza uharibifu wa misitu na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Rahima anasema upo umuhimu wa jamii kujikita katika kufuga nyuki kusaidia kuhifadhi na kusimamia rasilimali misitu.

Anawaagiza wafugaji kutumia mbinu wanazofundishwa na kufuga nyuki kisasa kwa kutumia teknolojia ili kupata manufaa zaidi.

Mwenyekiti wa Bodi ya MJUMITA Rehema Ngelekela, anasema mtandao huo umehifadhi hekta milioni 1.8 za misitu iliyopo kwenye ardhi ya vijiji na kutoa fursa ya umiliki na usimamizi katika nyanja mbalimbali.





# India, Tanzania kushirikiana matumizi akili mnemba

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NCHI ya India imeahidi kuendeleza ushirikiano na Tanzania kwenye fursa mbalimbali ikiwamo matumizi ya akili mnemba na mafunzo ya uandishi wa sheria.

Balozi wa India nchini Tanzania, Bishwadip Dey, alisema hayo juzi alipotembelea Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali jijini Dodoma. Akizungumza mwishoni mwa wiki kwenye ofisi hiyo, Balozi Dey alishukuru kwa mapokezi na kuelezea fursa mbalimbali za kisheria zilizoko India ambazo Tanzania inaweza kunufaika nazo.

Alizitaja fursa hizo ni pamoja na mafunzo mbalimbali ya uandishi wa sheria, uaandaji wa maamuzi ya mahakama na usuluhishi wa migogoro nje ya mahakama.

Aidha, alizungumzia suala la matumizi ya teknolojia ya akili mnemba katika utekelezaji wa majukumu ya kisheria na kwamba ipo haja ya Tanzania kujifunza teknolojia hiyo ili kurahisisha shughuli mbalimbali za kisheria.

**"Teknolojia imekuwa kwa kasi kwenye masuala mbalimbali imani yangu kupitia ziara hii utakuwa mwanzo mzuri wa wataalamu hususani wa sheria kutoka Tanzania watapata fursa nzuri..."**

"Teknolojia imekuwa kwa kasi kwenye masuala mbalimbali imani yangu kupitia ziara hii utakuwa mwanzo mzuri wa wataalamu hususani wa sheria kutoka Tanzania watapata fursa nzuri ya kujifunza matumizi ya teknolojia katika kuendesha shughuli za kisheria, hivyo kurahisisha utendaji kazi wao." Alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwandishi Mkuu wa Sheria, Onorius Njole, alisema ziara hiyo ni mwendelezo wa kuimarisha ushirikiano ulipo kati ya Tanzania na India pamoja na uhusiano wa kidiplomasia.

Alimshukuru balozi huyo kwa kufika kwenye ofisi hiyo kujitambulisha na kufanya mazungumzo kuhusu masuala mbalimbali ya ushirikiano.

Alisema ni matumaini yake kuwa ziara hiyo itabainisha fursa mbalimbali ambazo zitendeleza ushirikiano kati ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na India. Alisema: "Mheshimiwa Balozi tunakukaribisha sana kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, natumaini kupitia ziara hii ofisi yetu itaweza kufahamu masuala mbalimbali ya kisheria yanavyotekelezwa India, pia ni fursa nzuri ya kubadilishana uzoefu na kuendeleza ushirikiano baina ya nchi hizi mbili."



Mkuu wa Wilaya ya Mkalama mkoani Singida, Moses Machali, akizungumza jana na wananchi wa Kata ya Nduguti wilayani humo, wakati wa bonaza la uchaguzi wa serikali za mitaa lililofanyika kwenye viwanja vya Shule ya Msingi Nduguti. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# TSC yawaita walimu wenye kero, matatizo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TUME ya Utumishi wa Walimu (TSC), imewataka walimu kujitokeza kutatuliwa kero zinazowakabili katika kliniki ya siku saba inayoendeshwa na tume hiyo jijini Dodoma.

Akizungumza na waandishi wa habari, Katibu wa TSC, Paulina Nkwama alisema hatua hiyo ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Walimu Duniani ambayo hufanyika Oktoba kila mwaka.

Paulina alisema mwisho wa kliniki hiyo ni Oktoba 11, mwaka huu, kwamba ni ya muhimu hivyo walimu wanakaribishwa kufika kwa ajili ya kupata elimu na kueleza kero zao.

Alisema TSC ni mdau muhimu katika kuadhimisha Siku ya Walimu Duniani kwa kuwa walimu walioajiriwa katika utumishi wa umma wanaofundisha kwenye shule za msingi na sekondari Tanzania Bara wanahudumiwa na tume hiyo.

"Tume inahudumia walimu 274,541 ambao walimu wa shule za msingi ni 180,325 na 94,216 ni wa shule za sekondari," alisema.

Alisema serikali kupitia TSC inavyoshughulikia maslahi ya walimu katika kipindi cha serikali ya sasa walimu 37,473 wameajiriwa na kupangiwa vituo vya kazi katika mamlaka za serikali za mitaa.

"Kwa kipindi cha mwaka 2020/21 walimu waliopandishwa vyeo ni 126,346, mwaka 2021/22 waliopandishwa vyeo ni 35,112, mwaka 2022/23 ni 65,925 na mwaka 2023/24 walipandishwa vyeo 158,916. Katika kipindi hicho walimu 25,006 wamepandishwa vyeo baada ya kujiendeleza kielimu," alisema Nkwama.

Pia, alisema kuwa tume hiyo imefanya ziara shuleni kwa ajili ya kutoa elimu na ufafanuzi wa maadili katika utumishi wa walimu, ili kuwawezesha kuelewa wajibu na haki zao kwa lengo la kuwaepusha kufanya makosa yanayosababisha kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

Alisema serikali kupitia mradi wa boost imeipatia tume magari 11 kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma kwa walimu ngazi ya wilaya na makao makuu.

# Masauni: Tutatatua changamoto za vyombo vya usalama

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamadi Masauni, amesema wizara itahakikisha inafanyia kazi na kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazovikabili vyombo vya usalama vilivyo chini yake.

Alisema hayo wilayani Kongwa wakati akipokea ripoti ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika eneo hilo, kusema katika hatua za kutatua changamoto ya vitendea kazi Novemba mwaka huu wizara itapokea vifaa vitakavyoelekezwa katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Waziri Masauni alifanya ziara ya kikazi wilayani humo iliyoenda sambamba na uzinduzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa mkoani Dodoma ikiwamo ujenzi wa vituo vya polisi, shule ya sekondari pamoja na maabara zake.

Pamoja na mambo mengine, Waziri Masauni alipokea changamoto mbalimbali zinazokwamisha vyombo vya usalama.

"Kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji tutapokea vitendea kazi mbalimbali yakiwamo magari ya kuzima moto, helikopta na boti, lengo likiwa ni kuboresha huduma zinazotolewa na jeshi hilo katika kuokoa na kukabiliana na majanga mbalimbali," alisema.

Aliongeza kuwa moja ya jambo alilobaini kwenye ziara ni kuona watendaji wa vyombo vya usalama vilivyo chini ya wizara yake kufanya kazi kwa ufanisi ili kuhakikisha amani na usalama inakuwapo wakati wote.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alilipongeza Jeshi la Polisi kwa utendaji mzuri wa majukumu yake ya kuzuia uhalifu nchini.

Katika hatua nyingine, Kamati ya Usalama ya Wilaya ya Kongwa iliridhishwa na utendaji wa Mkuu wa Magereza pamoja na Ofisa wa Usajili Wilaya kwamba wamekuwa wakitekeleza majukumu ya kijamii kwa ufanisi na kuleta mabadiliko makubwa katika eneo hilo.

# JKT: Leteni watoto wapate mafunzo ya uzalendo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMANDA wa Kikosi 834 KJ Makutopora, Kanali Festo Mbanga, amewahamasisha Watanzania kuwapeleka watoto kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), ili wapate mafunzo yatakayowajenga kuwa wazalendo, wajasiriamali na wakakamavu.

Alisema hayo jijini hapa alipokuwa akizungumza na kikundi cha Operesheni Kambarage kilichopitia mafunzo katika kikosi hicho mwaka 1990 hadi 1991 baada ya kutembelea kambini hapo na kufanya shughuli mbalimbali ikiwamo upandaji wa miti.

"Watanzania hamasisheni kuwapeleka watoto kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), ili waweze kupatiwa mafunzo yatakayowajengea upendo, uzalendo, ujasiriamali na ukakamavu ili waweze kukabiliana na changamoto za maisha," alisema.

Alisema ujio wa kikundi hicho imekuwa chachu kwao jambo ambalo linaonesha kuwa wapo baadhi ya watu waliopitia mafunzo ya JKT na yamewasaidia katika maisha yao.

Mmoja wa viongozi wa kikundi hicho, Vivian Komu alisema kuwa lengo la kutembelea kikosi hicho ni kuyaenzi mafunzo waliyoyapata miaka 33 iliyopita, yamewasaidia kutekeleza majukumu yao kwa weledi na uzalendo kwa maendeleo ya Taifa.

"Mafunzo tuliyoyapata mwaka 1990 mpaka 1991 hapa Makutopora yametufaa sana katika maisha yetu na taifa kwa ujumla, kwamba mpaka leo tunakutana hapa kila mmoja anamajukumu yake na ukweli ni kwamba nidhamu, uzalendo na ukakamavu wetu ni matokeo ya kupitia mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa," alisema Komu.

Kiongozi mwingine, Frida Marco alisema taifa lipo salama kwa sababu ya kuwa na vijana wengi wanaopitia jeshini, hivyo aliwaomba wazazi wasiwafiche watoto pindi wanapotakiwa kujiunga na jeshi.



# Prof. Kabudi atoa maagizo uzalishaji wa pareto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imeagiza Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, kufanya utafiti na kuzalisha mbegu bora za pareto kisha kuzisambaza kwa wakulima ili kuongeza tija ya uzalishaji wa zao hilo.

Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi, alitoa agizo hilo juzi kwenye mkutano wa hadhara na wananchi wa Kata za Santilia, Isuto na Iyunga Mapinduzi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Prof. Kabudi alifanya mkutano huo ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake katika halmashauri zote za Mkoa wa Mbeya ambako anazindua miradi ya maendeleo, kuweka mawe ya msingi kwenye miradi mipya na kusikiliza kero za wananchi.

Alisema ili wananchi waongeze uzalishaji wa zao hilo wanatakiwa kusaidiwa mbegu za kisasa na mbinu bora za kilimo na hivyo akakiagiza kituo hicho kuhakikisha kinazalisha mbegu za kutosha na kuzisambaza kwa wakulima.

"Lakini pia maofisa ugani hakikisheni mnawafahamu vizuri wakulima, hakikisheni mnakusanya taarifa za wakulima wenu, mjue mahali walipo, ukubwa wa mashamba yao na mahitaji yao ili muwahudumie vizuri," alisema Prof. Kabudi.

**"Lakini pia maofisa ugani hakikisheni mnawafahamu vizuri wakulima, hakikisheni mnakusanya taarifa za wakulima wenu, mjue mahali walipo, ukubwa wa mashamba..**

Alisema serikali imekuwa ikitoa ruzuku ya mbolea na pembejeo mbalimbali za kilimo ili kuwapunguzia wakulima gharama za uzalishaji na kuongeza tija.

Aidha, aliagiza uongozi wa Mkoa wa Mbeya, kushirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha bei ya zao hilo inaongezeka ili wakulima wanufaike na hata serikali inufaike kwa kukusanya mapato yatokanayo na mauzo ya zao hilo.

Hata hivyo, aliwataka wakulima wa zao hilo kuacha kuchuma maua machanga na kuanika pareto kwenye vumbi akidai kuwa vitendo hivyo vinachangia kushusha thamani ya zao hilo.

Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza alisema Mkoa wa Mbeya ndio unaoongoza nchini kwa uzalishaji wa pareto na kwamba asilimia kubwa ya zao hilo linazalishwa katika halmashauri hiyo.

Alisema changamoto inayowakabili wakulima wa zao hilo ni bei kuwa ndogo ambapo alisema mpaka sasa wakulima wanaendelea kuuza zao hilo kwa Sh. 3,800 kwa kilo moja bei ambayo alisema imedumu kwa muda mrefu.

Alisema thamani ya Dola kwa sasa imepanda lakini bado wakulima wanauza pareto kwa bei ndogo ikilinganishwa na mataifa mengine jirani ikiwamo Kenya.

Hivyo, aliiomba serikali kuwasaidia wakulima wa maeneo hayo kuongeza bei ili iendane na gharama za uzalishaji na wananchi wengi zaidi wahamasike kuzalisha zao hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alisema wanaendelea na mazungumzo na wanunuzi wa zao hilo ili kuongeza bei ya zao hilo ambapo alisema wanaendelea na vikao na wadau mbalimbali wa zao hilo.

Alisema uzalishaji wa zao hilo unaongezeka kila mwaka na kwamba lengo la serikali ni kufikia uzalishaji wa zaidi ya tani 6,000 msimu ujao wa kilimo.



Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi, akiwahutubia wananchi wa Kata ya Santilia katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya juzi, alipofanya ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi ya mkoa huo, na kuzindua Kituo cha Afya Santilia. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mahakama inayotembea yazinduliwa Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya imezindua huduma ya mahakama inayotembea kupitia gari maalumu litakalokuwa likizunguka maeneo mbalimbali kwa lengo la kurahisisha utoaji huduma.

Uzinduzi huo ulifanyika mwishoni mwa wiki katika Kituo cha Mabasi cha Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wakiwamo wananchi viongozi wa serikali ya mkoa.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya, Joachim Tiganga alisema uzinduzi wa huduma hiyo ni moja ya juhudi za serikali kupitia mahakama za kufanya maboresha katika utoaji huduma za kisheria kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kusogeza huduma mahali walipo.

Vilevile alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa mpango wa mahakama wa mwaka 2021/2025 wa kuhakikisha wananchi wasioweza kuzifikia huduma za kimahakama wanafikiwa ili wapate haki zao.

"Kupitia huduma hii wananchi wengi sasa wanayo nafasi ya kuifikia mahakama yetu na kupata huduma kwa muda mfupi sana, wataweza kufungua kesi zao na zitasikilizwa na kukamilika," alisema Jaji Tiganga.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alipongeza kuanzishwa kwa huduma hiyo kwa maelezo kuwa wapo baadhi ya wananchi hawana uwezo wa kwenda mahakama za wilaya na mwanzo.

Alitoa wito kwa wananchi kuitumia mahakama hiyo kwa ajili ya kuwasilisha kesi zao ili zifanyiwe kazi, huku akiitaka mahakama hiyo kutumia huduma hiyo kuhakikisha wananchi wengi wanayafikia maeneo yote.

Mmoja wa wananchi, Kisonga Hamis aliomba mahakama watumie huduma hiyo kutoa elimu kwa wananchi kuhusu shughuli za mahakama kwani wengi hawana uelewa wa kutosha kuhusu mahakama na wengine wanaogopa kuifikia kutokana na mtazamo hasi.

# Vijana waandaliwa kufanya kazi Mchuchuma, Liganga

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

SERIKALI imesema inatumia vyuo vilivyoko mkoani Njombe, kuwaandaa vijana katika fani mbalimbali zikiwamo za ufundi, ili waitumie kujiajiri na kuajiriwa kwenye miradi ikiwamo mradi wa Liganga na Mchuchuma.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipotembelea na kukagua ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) kilichoko katika Wilaya ya Ludewa kinachojengwa kwa Sh. bilioni sita.

Alisema malengo ya serikali kujenga chuo hicho ili vijana wapate ujuzi utakaosaidia kupata ajira kupitia mradi huo.

Alisema kuwa maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kwamba elimu inayotolewa iwe na ujuzi ili kumwezesha mtoto anapomaliza shule aweze kufanya shughuli zake mwenyewe.

Naye Mbunge wa Ludewa, Joseph Kamonga aliwahamasisha wazazi kuwapeleka watoto wao kwenye vyuo vya ufundi stadi ili kupata elimu itakayowasaidia kutumika kwenye mradi huo.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Anthony Kasore, alisema kupitia mradi wa Liganga na Mchuchuma wamejipanga kuhakikisha wanatengeneza vijana wenye ujuzi na watakaoshiriki vema kwenye miradi huo.

"Tuko tayari na ndiyo maana chuo kipo huku kwa ajili ya kusogeza huduma na kuwapatia wananchi ujuzi unaotakiwa ili kushiriki vema katika hili eneo," alisema Kasore.

Alisema chuo hicho kitakuwa na uwezo wa kuchukuwa wanafunzi 640 kwa wakati mmoja kwenye mafunzo ya muda mrefu lakini zaidi ya wanafunzi 1000 kwenye kozi fupi.

Nao baadhi ya wanafunzi akiwemo, Nashon Hashimu aliwataka vijana kujiunga na ufundi kwa sababu utawasaidia kukabiliana na tatizo la ajira.

Pia waziri huyo alizindua nyumba za walimu katika Shule ya Sekondari Luponde, ambapo Diwani wa Kata Lubonde, Edgar Mtitu aliomba serikali kuwasaidia kujenga bweni la wanafunzi wa kiume ili waondokane na adha ya kutembea umbali mrefu.

# Mwongozo 'kuyabana' mashirika kutoa gawio wakamilika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISI ya Msajili wa Zanzibar imesema kukamilika kwa mwongozo wa mashirika ya umma itawezesha mashirika hayo kujiendesha kibiashara na kutoa gawio kwa serikali.

Msajili wa Ofisi hiyo, Wahid Mohammed Sanya, alisema hayo juzi visiwani hapa wakati akifungua mkutano wa kupokea maoni ya wadau kwa ajili ya mwongozo wa uandaaji wa mpango mkakati (SP) kwa mashirika ya umma.

Alisema hivi sasa mashirika mengi yamekuwa hayajiendeshi kibiashara hali ambayo inasababisha serikali kukosa gawio.

Aidha, alisema yote hayo wanayafanya kwa lengo moja la kuona mashirika ya umma yanaweza kusimamiwa vizuri, kufanya biashara na kutoa huduma bora ili serikali iweze kupata kinacho stahiki.

Alisema kuwa na mwongozo mmoja kwa mashirika ya umma inasababisha mashirika hayo kwenda katika utaratibu mzuri na kuanza kutoa matokeo mazuri kwa baadaye.

Alisema kuna upungufu ambao ulikuwa ukijitokeza kabla ya kuwepo kwa ofisi ya msajili wa hazina, kulikuwa hakuna mwongozo wa uandaaji wa mpango mkakati wa mashirika ya umma.

Sanya alisema serikali ilikuwa inamwongozo wake umeandaliwa na tume ya mipango lakini kwa mujibu wa Sheria Msajili wa Hazina anatakiwa kutengeneza mwongozo kwa mashirika yake ya umma.

Mkurugenzi wa Mitaji ya Umma na Uwekezaji, Ramia Mohamed Ramia na Mkuu wa Kitengo cha Sheria wa Ofisi hiyo, Mustafa Omar Abdallah, walisema lengo la kikao hicho ni kutekeleza matakwa ya sheria kuwa na mfumo mmoja wa mwongozo kwa mashirika hayo utakaoendana na malengo makuu endelevu ya nchi.

Walisema Msajili wa Hazina kwa mujibu wa sheria anatakiwa kuanzisha mwongozo huo, hivyo ni imani yao kuwa mkutano huo utawawezesha kuyatekeleza yale yote yaliyokuwapo katika mwongozo huo.

Ofisa Mitaji ya Umma na Meneja Miundo na Maslahi Ofisi ya Msajili wa Hazina, Abdullah Salum Abdullah, alisema mwongozo huo umelenga kutoa njia ya mpango mikakati na kuziwezesha taasisi za umma kuweka malengo yake na kuyafikia.

Alisema kupitia mwongozo huo mashirika yataweka malengo kulingana na sera za nchi na kufanya tathmini ya utekelezaji wa kazi zao kwa urahisi.

Alisema ni lazima sasa mashirika kubadilika na kuandaa mpango kazi ili kuweza kukamilisha malengo yao vizuri, kwamba bila ya mwongozo ni vigumu kutekeleza majukumu yao.

Abdulaziz Mohammed Ramia kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) na Salum Mbwana Juma kutoka Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) waliahidi kuuchukua mwongozo huo na kuufanyia kazi kwa mujibu wa sheria, ili lengo lililokusudiwa liweze kutimia.

# UWT: Rais Samia atastaafu kwa heshima

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

UMOJA wa Wanawake (UWT) Mkoa wa Kaskazini Unguja umesema Rais Samia Suluhu Hassan atamaliza salama vipindi vyake vya uongozi kwa mujibu wa kikatiba, kustaafu kwa heshima kama walivyofanya watangulizi wake.

Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Kaskazini Unguja, Maryam Muharram Shomari, aliyasema hayo Mahonda Mkoa wa Kaskazini Unguja wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu masuala yanayoendelea katika mitandao ya kijamii.

Alisema Rais Samia amekabidhiwa taifa kuliongoza, kwamba haongozi nchi kwa utashi wa mitandao ya kijamii.

Aliitaja Tanzania nchi tukufu inayoheshimu sheria na katiba, muda wa kiongozi wa kuingia na kutoka madarakani ni matakwa ya kikatiba, hayupo wa kubadilisha utaratibu huo.

"Ukiwa kiongozi tarajia dhoruba na misukosuko. Hata jahazi kupata kwake dhoruba siyo mwisho wa safari. Nahodha jasiri hajitosi baharini hufika salama na kutia nanga," alisema Shomari.

> **Alisema: "Awamu ya kwanza hadi ya tano tulianza na kumaliza pamoja. Kinga yetu ni mshikamano na kutoganyika. Binadamu kwa mwanamke siyo tafsiri ya udhaifu".**

Aidha, alisema uongozi wa Rais Dk. Samia umefanikiwa katika maendeleo ya kisekta na ni mfano katika utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM.

Alisema: "Awamu ya kwanza hadi ya tano tulianza na kumaliza pamoja. Kinga yetu ni mshikamano na kutoganyika. Binadamu kwa mwanamke siyo tafsiri ya udhaifu".

Alisema kiti cha urais kina thamani ya juu, nguvu zitokanazo na ridhaa hivyo amewataka wanaokitania kiti hicho wafahamu utukufu na hadhi yake. "Maoni katika mitandao ya kijamii ni kielelezo cha Tanzania kuna uhuru wa maoni. Wanaotoa maoni acha wafanye hivyo lakini kuna mipaka na hawana uwezo wa kubadili lolote," alisema.

Kadhalika, alimpongeza Rais Samia anavyotimiza majukumu yake kwa kusimamia misingi iliyowekwa na waasisi wa taifa kwa ujasiri na uthubutu.




Watoa mada kutoka Deloitte Health Forum wakielezea mafanikio ya miradi ya USAID Afya Yangu Kanda ya Kusini na USAID Kizazi Hodari kwenye Jukwaa la Afya lililoandaliwa na Deloitte kwa msaada wa PEPFAR wakati wa Mkutano wa 11 wa Afya Tanzania (THS) uliofanyika Zanzibar mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jaji azitaka taasisi kuwaunga mkono wajane

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JAJI wa Mahakama Kuu Zanzibar, Fatma Hamid Mahmoud, amezitaka taasisi za serikali na binafsi kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Jumuiya ya Wajane Zanzibar (ZAWIO) katika kuwawezesha na kuwainua wajane kiuchumi.

Alisema hayo juzi wakati akifungua mafunzo ya wajane wanaofanya biashara katika Soko la Jumbi na Mombasa Unguja.

Alisema mashirika na taasisi nyingi zinatoa kipaumbele zaidi kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu na kulisahau kundi la wajane ambalo linahitaji kusaidiwa kwa kiasi kikubwa.

Aidha, alisema pamoja na kuwa wajane wanaweza kuingizwa katika kundi la wanawake lakini baadhi yao wanajitegemea wenyewe na wengi wao hawana kazi za uhakika za kuwapatia kipato cha kuendeleza maisha yao kila siku.

Hata hivyo, alisema kutokana na changamoto mbalimbali wanazozipata kuna uwezekano mkubwa wa kundi hilo kujiingiza katika mambo yasiofaa ili kukidhi mahitaji yao.

"Tunajua kuna kundi la wajane ambao wanapata matatizo ya akili kutokana na msongo wa mawazo kwa kushindwa kukabiliana na shida za maisha na lakini hata pia wengine kujiingiza katika masuala ya mapenzi," alisema Jaji Fatma.

Hata hivyo aliipongeza taasisi ya wajane kwa kuanzisha programu maalumu za kuwasaidia kufanya shughuli za uchumi kwa kuwaunganisha na taasisi za kibenki ili kuwapatia mitaji.

Naye Mkurugenzi wa ZAWIO, Tabia Makeme Mohammed, alisema mafunzo hayo yamejikita zaidi kuwapatia elimu ya mbinu za kuanzisha na kuendeleza biashara. Pia yamejikita kujua fursa mbalimbali zilizoko kupitia jumuiya hiyo na kujikinga na maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi na magonjwa ya afya ya akili. Aidha, alisema mafunzo hayo pia yatawasaidia kujua haki zao za msingi ikiwamo taaluma juu ya afya ya akili, utawala wa sheria, usawa wa vyombo vya dola na kugombania nafasi mbalimbali za uongozi.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo walisema watayafanyia kazi mafunzo waliyopewa ikiwamo kujikinga na VVU pamoja na afya ya akili.

Asha Ali miongoni mwa washiriki wa mafunzo hayo aliwataka wajane wenzake wasijiweke nyuma, wajitambue, wafanye kazi kwa bidii na wasikubali kurubuniwa na watu wasiopenda maendeleo yao.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**AFRA SELBARD MHAGAMA** anatangaza kupotea kwa cheti cha chuo (Diploma Level 5) chenye namba IRDP/TCCD/SE21/0228 kilichotolewa na Chuo cha Mipango (Institute of Rural Development Planning) mwaka 2022. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/DOD/43964/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ESTHER AMOS MASASI**

ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T 902 BWM AINA YA TOYOTA PREMIO , CHASSIS NO. AT2110083552, ENGINE NO. 7AH096993. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI:
**DOD/DOD/RB/371323/2020**

## KUPOTEA KWA KADI YA GUTA

**MAGRETH LENALD MNG'ONG'O**

ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GUTA AINA YA WANHOO GUTA YENYE USAJILI NAMBA MC 317CAJ, CHASSIS:LW8HDMZ40JW011076 NA ENGINE:WH163MLB180573860. KWA YEYOTE ATAKEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

POLISI TAARIFA: RB NO.
**PHQ/NJO/4272/2024**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 39 LA 2016**
**PRISCA PROTUS TUMBO.........MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**

- **REV. SAMSON SWILA**
- **HABIBA ALLY**
- **NASSORO**
- **FLORA MANGULA................MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**
- REV. SAMSON SWILA (3) NASSORO
- HABIBA ALLY (4) FLORA MANGULA

**POPOTE ULIPO/MLIPO**
**PRISCA PROTUS TUMBO** amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 9/10/2024 saa 03:00 asubuhi mbele ya Mh. J.W. SILLAS. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hii leo tarehe 20 Mwezi 09, 2024

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.22849 OF 2024**
**IN the Matter of the late**
**JANECECILIA RAYMOND HAULE**

**1. OMARI LUGONGO NGUNGWE**
**2 ............................................**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above- named pepetitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 10th day of OCT,2024.
Dated at Morogoro this 02nd day of OCT 2024.

..................................
**RESIDENT MAGISTRATE**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo wilaya ya Shinyanga**
**Kituo cha: Kizumbi Mkoa Shinyanga**
**Shauri la Madai. Na 24/2024**
**Jina la Mdai: Hizza Ramadhan Mambo**
**Jina la Mdaiwa: Kassim Issa Swalehe**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 kanuni za taratibu madai katika Mahakama ya Mwanzo)**

**Kwa................ Kassim Issa Swalehe**
**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba(eleza hapa habari za madai) MADAI YA TSH. 11,285,000/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 17 mwezi 10 mwaka 2024 saa 08:00 asubuhi, kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO**:kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitaka kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusilikiza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa na Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 7 mwezi wa 10 mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO - KIZUMBI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANI**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA)**
**Mahakama ya mwanzo ARUSHA MJINI**
**Wilaya ya ARUSHA**
**MADAI NAMBARI 160 YA 2024**
**Mdai............ PETRO MARODA**
**Amdai**
**Mdaiwa ............NASINYINYARI LAWASARE KIVUYO**
**Kwa .........ASINYARI LAWASARE KIVUYO- ARUSHA**

**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta /wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za madai):**
**FIKA BILA KUKOSA ILI KUJIBU MADAI YA TALAKA**

Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajika kuhudhuria mahakama hii siku ya ALHAMIS tarehe 17/10/2024 saa 2:30 asubuhi/alasiri kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo .
Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 3/10/2024

..................................................
**Hakimu /Hakimu Mkazi/Mahakama ya Mwanzo**

---

**DAWN AFRICA TANZANIA LIMITED**

**Company No. 99212**
**(UNDER VOLUNTARY LIQUIDATION)**
**FINAL MEETING AND DISSOLUTION**
**(Made under Section 345 (1) & (2) of The Companies Act Cap 212 RE: 2019)**

NOTICE IS HEREBY GIVEN to the GENERAL PUBLIC that DAWN AFRICA TANZANIA LIMITED is undergoing Voluntary Liquidation and it has called for a Final Meeting and Dissolution of the Company which is intended to be held at the REGISTERED OFFICES OF THE COMPANY 1/1B SAM NUJOMA ROAD, MIKOCHENI LIGHT INDUSTRIAL AREA, KINONDONI, DAR ES SALAAM on the 15th _of_ November_2024 at 10:00 AM.

DATED THIS_30th_DAY OF_ September 2024.

HASHIM RWENYAGIRA JABIL
HOUSE NO.34, SINDANO STREET,
MWANANYAMALA, KINONDONI,
P.O. BOX 8809, DAR ES SALAAM.

---

**OFISI ZA MATANGAZO**
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0677020701
E-mail: advertise@guardian.co.tz,
Website: www.ippmedia.com

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# 40 wauawa shambulio la Hamas Israel

**JERUSALEM,** Israel

WAKATI Israel ikisherehekea mwaka mmoja tangu mashambulizi ya kundi la Hamas katika taifa hilo, Oktoba 7, 2023, kundi hilo limefanya tena shambulizi la kushtukiza nchini humo na kusababisha vifo vya takriban watu 40.

Ilielezwa kuwa shambulizi hilo la kushtukiza lilitekelezwa jana asubuhi, huku takwimu hizo zikitolewa na kitengo cha Israel cha magari ya kuwabeba wagonjwa ikisema kuwa idadi hiyo inajumuisha watu waliouawa kwa kudondokewa na roketi na katika hujuma za ardhini.

Ilibainishwa kuwa Hamas ilifyatua roketi 2,200 kutokea Ukanda wa Gaza, katika kile ilichokitaja kuwa ni operesheni ya kijeshi.

Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, alisema nchi yake iko vitani, na kwamba maadui wa Israel watalipa gharama kubwa kwa kiwango ambacho hakijawahi kushuhudiwa.

Aidha, pande mbalimbali duniani, zikiwamo Marekani, Umoja wa Ulaya (EU) na Jumuiya ya Kujihami ya (NATO) zililaani mashambulizi hayo ya Hamas, huku ikisisitiza mshikamano na Israel pamoja na watu wake.

Rais wa Mamlaka ya Wapalestina, Mahmoud Abbas, alisema Wapalestina wanayo haki na kujilinda, huku Saudi Arabia na Misri zikizitaka pande zote kuwa na ustahimilivu.

Wakati huohuo, Wizara ya Afya ya Gaza ilisema kuwa karibu watu 200 wameuawa, huku 1,600 wakijeruhiwa baada ya mashambulizi yaliyofanywa na Jeshi la Israel katika ukanda huo kama hatua ya kujibu mashambulizi.

Wakati hayo yakijiri, kupitia chapisho la kwenye mtandao wa X, Kiongozi Mkuu wa Iran Ayatollah Ali Khamenei (pichani), alisema mashambulizi yaliyoongozwa na Hamas ya Oktoba 7 mwaka jana huko Israel yaliurudisha nyuma utawala wa taifa hilo kwa miaka 70 nyuma.

Ilielezwa kuwa Khamenei aliongoza mahubiri adimu mjini Tehran siku ya Ijumaa ya kukumbuka mauaji ya kiongozi wa Hezbollah Hassan Nasrallah mwezi uliopita, huku akisifu shambulio la Hamas la Oktoba 7 akisema kuwa ni halali.

Pia ilielezwa kuwa Hamas na Hezbollah ni sehemu ya mhimili wa upinzani wa Iran, muungano wa makundi ya wapiganaji wa Kiislamu yanayozunguka Iraq, Syria, Lebanon, Gaza na Yemen. **DW, CNN**



# Ombi la Gachagua lakataliwa

**NAIROBI,** Kenya

MAHAKAMA Kuu nchini Kenya kwa mara ya pili imekataa kutoa amri ya kusitisha kesi ya kumfukuza Naibu Rais, Rigathi Gachagua, ambaye siku chache zilizopita aliwasilisha ombi la kusitisha mchakato huo kwa madai kwamba kuna kanuni muhimu zilipuuzwa.

Kesi hiyo ilitajwa Jumatatu mbele ya Jaji Bahati Mwamuye, ambaye aliagiza shauri lililowasilishwa na Cleopas Malalah lifikishwe mbele ya Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu, Chacha Mwita kwa maelekezo zaidi.

Wakati huo huo katika ombi la kutaka masuala yote ya kupinga mchakato wa mashtaka kuunganishwa, Bunge lilisema kuwa jambo hilo linaibua hoja sawa na zinapaswa kuunganishwa ili kuhojiwa na mahakama ili kuendeleza uondoaji wa malalamiko kwa ufanisi na haraka.

"Kufikia sasa mbele ya Mahakama Kuu ya Nairobi na vituo vingine nchini kote kuna maombi 13 yote yakipinga kuondolewa kwa Gachagua kama Naibu Rais wa Jamhuri ya Kenya," sehemu ya nyaraka ya mahakama ilisema.

Pia ilielezwa kuwa Septemba 30, mwaka huu mahakama ilikataa kutoa maagizo ya kusitisha bunge kushughulikia ombi la kuondolewa mashtaka dhidi ya Naibu Rais Rigathi Gachagua.

Ilielezwa kuwa hoja iliyowasilishwa na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha (UDA) Cleophas Malala, ililenga kuzuia Bunge la Kitaifa na Seneti kuwasilisha, kujadili, kuzingatia au kufanyia kazi hoja yoyote ya kutaka kumtimua Gachagua.

Malala alisema kuwa mabunge yote mawili hayana kikomo kinachohitajika cha kanuni ya kijinsia ya theluthi mbili na hivyo yamekiuka masharti ya katiba.

Katika hatua nyingine, akizungumza katika mjadala kwenye runinga ya Citizen jana, Wakili Steve Ogola alitoa maoni kwamba ombi la Naibu Rais Gachagua la kuomba msamaha kutoka kwa bosi wake Rais William Ruto linaweza kuchukuliwa kama kukiri hatia.

"Kuomba msamaha ni kukiri wazi kuwa na hatia. Hatuwezi kujadili ubora wa kuomba msamaha," Ogola alisema.

Naibu Rais, ambaye atafika mbele ya bunge leo kujitetea, anatuhumiwa kwa utovu wa nidhamu, ukiukaji wa katiba, ufisadi na madai ya kutomtii bosi wake Rais Ruto.

Kwa mujibu wa wakili Ogola, Gachagua ana hatia ya tuhuma zinazotolewa dhidi yake.

"Ikiwa anaomba msamaha katika muktadha wa mashtaka yanayosubiri dhidi yake, ni lazima tuchukue msamaha huo kwa maana yake, ni kukiri hatia," anasema wakili huyo.

Katika utetezi wake pia, Naibu Rais anayekabiliwa na matatizo alisema sehemu ya mali ya mabilioni ya shilingi inayohusishwa naye ni ya marehemu kaka yake aliyekuwa Gavana wa Nyeri, Nderitu Gachagua. **Citizen**



Daktari wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), akimchoma mtoto chanjo ya Mpox, huku ikielezwa kuwa dozi za chanjo takribani 265,000 zimezinduliwa nchini humo. **PICHA: MTANDAO**

# DRC yazindua kampeni ya chanjo

**KINSHASA,** DRC

KITUO cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa Barani Afrika (Africa CDC) kimeipongeza Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kwa kuzindua chanjo ya ugonjwa wa Mpox, katika hatua za kukabiliana na maradhi hayo nchini humo.

Mkurugenzi Mkuu wa Africa CDC, Dk. Jean Kaseya, alisema jana kuwa ujio wa dozi takribani 265,000 za chanjo ya Mpox nchini humo, ni hatua muhimu kwa DRC kudhibiti kusambaa kwa ugonjwa huo.

"Africa CDC kinaipongeza DRC kwa hatua hiyo muhimu yenye kuashiria nguvu ya uongozi katika sekta ya afya hususani kwa kutilia mkazo watu walio katika mazingira hatarishi," alisema Dk. Kaseya.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, kituo chake kitaendelea kufanya kazi kwa karibu na DRC ili kuhakikisha kuwa chanjo hizo zinawafikia wahitaji kwa wakati muafaka ili kuzuia milipuko mingine.

"Kipaumbele chetu ni kutoa chanjo zenye ufanisi zaidi," alisema Dk. Kaseya.

Mpox ni ugonjwa wa virusi unaopatikana kwa wanyama (Nyani), kutokana na shughuli za kibinadamu. Na kwamba hutoka kwa wanyama na kuhamia kwa binadamu na kusababisha kuambukizana kutoka kwa binadamu mmoja hadi mwingine. **TRT**

# KIFARU AANZA TAMBO MTIBWA IKIZIDI KUCHAPA CHAMPIONSHIP

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Mtibwa Sugar ikiendelea kutoa vipigo kwenye Ligi ya Championship ambapo juzi ilipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Mbeya City, Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Thobias Kifaru, ametamba kuwa wamekwenda kutalii tu kwenye ligi hiyo.

Akizungumza baada ya mchezo huo uliochezwa juzi, Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro, Kifaru, alisema pamoja na kwamba walishuka daraja msimu uliomalizika, lakini kwa kiasi kikubwa wameweza kudhibiti wachezaji wao wengi kutohama, wakisajili wengine wazuri pamoja na kocha mzoefu, Melis Medo, hivyo wana uhakika wa kupanda Ligi Kuu msimu ujao na hakuna wakuwazuia.

"Huku tumekuja kutalii kwa muda, ukiangalia tayari tumeshashinda michezo mitatu na tuna pointi tisa, tunarejea kule ambako tumezoea, tutapanda bila kwenda kwenye 'play off', niwaambie mashabiki wa soka tu kuwa tunacheza msimu huu tu Ligi ya Champioship, halafu tunarejea Ligi Kuu," alitamba Kifaru.

**Mabao ya Mtibwa Sugar yalifungwa na Erick Kyaruzi na Raizin Hafidh, ushindi ambao umeifanya kuendelea kuongoza msimamo, ikifikisha pointi tisa, mabao sita ya kufunga na haijaruhusu bao katika wavu wake.**

Kwingineko Biashara United, ilipoteza mechi yake ya kwanza msimu huu, ilipochapwa bao 1-0 dhidi ya wenyeji wao, TMA, mchezo uliopigwa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, likiwekwa ndani ya nyavu na Abiud Mtambuka.

Bigman FC, ikiwa Uwanja wa Ilulu, Lindi, ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Green Warriors, bao lao likifungwa na Selemani Kibuta.

Mechi zingine zilizochezwa juzi, ni kati ya Mbeya Kwanza iliyokuwa nyumbani, Nangwanda Sijaona dhidi ya Cosmopolitan, ikishinda bao 1-0, Stand United nayo ilishinda ugenini bao 1-0 dhidi ya Mbuni FC, Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha, mapema, kabla ya mchezo mwingine wa Biashara na TMA.

Msenda Msenda ndiye aliyeifungia Stand United bao hilo pekee katika mchezo huo.

## *Mafunzo yatoa siri mvua ya magoli Mwenge*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya Klabu ya Mafunzo kuikaribisha Ligi Kuu Zanzibar timu ya Mwenge SC kutoka Kisiwani Pemba kwa kuwafunga mabao 5-0, imeanika siri ya kupata ushindi huo mzito.

Kwa ushindi huo walioupta Mafunzo juzi, Jumapili katika Dimba la New Amaan Complex, unawafanya kukwea kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo kwa kufikisha alama 10 sawa na Uhamiaji FC ambayo kwa sasa imeshuka hadi nafasi ya pili.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mchezo huo, Kocha Msaidizi wa Mafunzo, Abdalla Bakar, alisema siri kubwa ya ushindi huo ni ari waliyonayo wachezaji wenyewe tangu kuanza kwa ligi msimu huu.

Alisema baada ya kupoteza mchezo wao wanne, wachezaji walifanya bidii kubwa kuhakikisha hawapotezi mechi inayofuata jambo ambalo walilifanikisha.

Bakar alisema kushinda mchezo huo pia ni moja ya mipango yao katika kuhakikisha hawaachi alama kwenye michezo yao yote ya nyumbani.

"Kitu pekee tunachokishukuru ni wachezaji kuhamasika na lakini pia ari ya kupata matokeo mazuri kwa kila mchezo tunaocheza bila kuangalia matokeo yaliyopita, hii inatupa nguvu na moyo wa kufanya vizuri zaidi," alisema.

Aidha, alisema timu hiyo itaendelea kufanyia kazi kila kasoro au mapungufu wanayoyaona katika michezo yao bila kujali iwapo wameshinda.




Mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford (kushoto), akiwania mpira na beki wa kulia wa Aston Villa, Matty Cash, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Villa Park juzi na kumalizika kwa sare tasa. **PICHA: MTANDAO**

## Mkwasa: Hofu sababu kichapo Ngorongoro Heroes

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Vijana, Ngorongoro Heroes, Charles Boniface Mkwasa, amesema kupoteza kwa mabao 2-1 dhidi ya Rising Stars ya Kenya, juzi, katika mchezo wa ufunguzi wa michuano ya Afrika Mashariki na Kati chini ya miaka 20, kwa ajili ya kusaka tiketi ya kufuzu AFCON Kanda ya CECAFA, kumetokana na woga wa wachezaji wake.

Akizungumza baada ya kumalizika mchezo huo uliopigwa jioni, Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam, alisema wachezaji wake walionekana kuingiwa na hofu na kushindwa kucheza kama wenyeji wa michuano hiyo, kiasi cha kupoteza mchezo huo wa kwanza.

Mabao ya vijana wa Kenya chini ya miaka 20, Rising Stars katika mchezo huo yalifungwa na Kevin Wanganya na Andres Odhiambo, huku la Ngorongoro Heroes likiwekwa ndani ya nyavu na Rahim Mkinyange

"Kipindi cha kwanza hatukuwa kwenye ubora wetu wa kawaida, nahisi wachezaji wangu walikuwa na hofu kidogo kwa sababu Kenya walikuja tofauti na tulivyotegemea, wakawa wanacheza soka la nguvu, kwa maana hiyo wachezaji wangu walionekana kucheza kwa hofu.

Kipindi cha pili tulijitahidi kubadilisha, timu ilitulia, tukatoka kwenye mfumo wa kuweka viungo wachache kati, tukaongeza idadi, tukaongeza na wigo ya kushambulia, tukacheza na mastraika wawili, hiyo ikasaidia tukapata bao moja," alisema kocha huyo.

Hata hivyo, aliwatoa wasiwasi mashabiki wa soka nchini kuwa atakaa chini na vijana wake na kuwataka kuondoa hofu na kucheza kama wapo nyumbani.

"Niseme kama tusingekuwa na woga na hofu tungeweza kupata mabao mengi kipindi cha kwanza, kwa bahati mbaya hatukuwa na utulivu na umakini, lakini hatujakata tamaa, mimi ni mzoefu wa mashindano kama haya, unaweza ukafungwa mechi ya mwanzo na ukachukua kombe, naamini michezo ijayo tutakuwa vema na wachezaji watakuwa wametoa hofu na tutacheza kama timu mwenyeji," alisema.

Timu hiyo leo inatarajiwa kujitupa tena kwenye uwanja huo kucheza na Timu ya Taifa ya Djibouti, katika mechi ya Kundi A.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ALEXANDER-ARNOLD, MADRID

REAL Madrid walikuwa na mpango wa kumsajili beki wa England, Trent Alexander-Arnold, 25, kwa uhamisho wa bure msimu ujao wakati mkataba wake na Liverpool utakapokamilika, lakini huenda wakamnunua Januari baada ya beki wa Hispania, Dani Carvajal, 32, kupata jeraha baya la goti. ***(Sport)***

### LIVERPOOL NA MABEKI

LIVERPOOL inaendelea na mazungumzo ya mkataba mpya na mabeki wawili muhimu - Jarell Quansah mwenye miaka 21 na beki wa Ufaransa, Ibrahima Konate, 25. ***(Mirror)***

### POGBA KUJADILI NA JUVENTUS

PAUL Pogba,31, anajadiliana na Juventus kwa lengo la kumaliza msimu wake wa pili na klabu hiyo ya Serie A na kuanza upya baada ya marufuku yake ya kutumia dawa za kusisimua misuli kupunguzwa na Mahakama ya Usuluhishi wa Michezo, CAS. ***(Mail)***

### O'NEIL HATATIMULIWA

KLABU ya Wolves haina nia ya kumtimua kocha Gary O'Neil lakini itampa muda wa kubadilisha kikosi chake baada ya kupoteza mara sita katika mechi saba za mwanzo za Ligi Kuu England. ***(Telegraph)***

### CITY YATENGA MILION 80

KLABU ya Manchester City imetenga pauni milioni 80 kwa usajili wa wachezaji katika dirisha la Januari baada ya Rodri kujeruhiwa. ***(Football Insider)***

### PEREZ KUREJESHWA EPL

WEST Ham ina nia ya kumrejesha mshambuliaji wa zamani wa Leicester City na Newcastle United, Ayoze Perez, 31, kwenye Ligi Kuu England kwa matumaini kwamba mchezaji huyo wa Villarreal anaweza kuboresha safu yao ya mashambulizi. ***(Caught Offside)***

### XAVI ATAJWA MAN UNITED

KOCHA wa zamani wa Barcelona, Xavi anapigiwa upatu kuongoza mradi wa kujenga upya kikosi cha Old Trafford iwapo Erik ten Hag ataondoka Manchester United. ***(El Nacional)***

### DAVID AWINDWA BARCA

JARIBIO la Newcastle United kumsajili mshambuliaji wa Lille, Jonathan David, 24, limepata pigo baada ya Barcelona kuingia katika ofa ya kumtaka. ***(Shields Gazette)***


### EZE AGOMBEWA EPL

KLABU ya Liverpool imeungana na Newcastle United na Tottenham Hotspur katika mbio za kumnasa kiungo mshambuliaji, Eberechi Eze, 26, kutoka Crystal Palace. ***(Football Insider)***

### SANE AFUATILIWA BARCA

BARCELONA inamfuatilia winga wa Bayern Munich, Leroy Sane mwenye umri wa miaka 28, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Sport)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA ATOA SABABU EDERSON KUBAKI MAN CITY

**●●● Alijua tangu siku ya kwanza sitaki, hatukutaka lakini...**

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesema kwamba Ederson alibaki Manchester City wakati wa majira ya joto kwa sababu hakuna klabu iliyofika bei waliyotaka kumuuza kipa huyo.

**Ederson alikuwa akiwaniwa na Al Nassr na Al Ittihad za Saudi Arabia wakati wa dirisha la uhamisho.**

Lakini akizungumza baada ya mlinda mlango huyo wa Brazil kuokoa idadi kubwa ya mabao kusaidia City kushinda 3-2 dhidi ya Fulham Jumamosi, Guardiola alisema anafurahi kwamba ofa inayokubalika haikufikiwa.

"Alijua tangu siku ya kwanza sitaki, hatukutaka lakini ukweli, nitasema ukweli, ofa haikuja," alisema Guardiola.

Ederson ameshinda mataji sita ya Ligi Kuu England tangu awasili kutoka Benfica mwaka 2017. Ametajwa mara mbili katika timu bora ya mwaka ya Ligi Kuu na kushinda tuzo ya kipa bora kwa miaka mitatu mfululizo kati ya 2020 na 2022.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, amehifadhi nafasi yake kama namba moja wa City msimu huu, licha ya ushindani kutoka kwa Stefan Ortega, ambaye alitia saini mkataba mpya majira ya joto.

"Nilisema mara nyingi, ni miaka mingapi tuko pamoja? Miaka nane na Eddie. Mafanikio tuliyopata bila yeye, siwezi kuyaona, siwezi," alisema Guardiola.

"Tuna bahati kuwa naye. Tunatumaini, ana furaha."

# TEN HAG ALIA UKAME WA MABAO UTD



**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag amesema Manchester United lazima "iongeze nguvu" na kufunga mabao zaidi baada ya suluhu dhidi ya Aston Villa na kuendeleza mbio zao hadi mechi tatu za ligi bila kufunga bao.

United wamefunga mabao matano pekee katika mechi saba za ligi hadi sasa msimu huu na wameandikisha mwanzo wao mbaya zaidi katika kampeni tangu msimu wa 1989-90.

Ten Hag alisema yapo mazuri kwa timu kung'ang'ania na picha itaimarika tena watakapoanza kufunga mabao.

"Tunajua kwa wakati huu tuna upungufu wa mabao, kwa mtazamo huo si mwanzo mzuri, lazima tuongeze nguvu," alisema Ten Hag.

"Hilo ni eneo ambalo tunapaswa kuboresha. Lakini tuna michezo minne hatujaruhusu bao. Hiyo ni nzuri kwa sababu tunapaswa kulinda ipasavyo.

"Tumetengeneza nafasi nyingi katika mechi zetu saba, lakini lazima tuongeze kasi. Lazima tuzingatie Rasmus Højlund anarejea, bado anaendelea kuwa fiti, lakini wengine wanaongeza kasi. Nilifurahishwa na Marcus. Rashford, pia Alejandro Garnacho ni mzuri sana, na Antony.

"Itakuja. Kuna sababu zaidi, wakati mwingine ni kiwango. Tunawaamini wachezaji na siku moja itakuwa poa."



# Postecoglou: Kipigo kibaya kwa Spurs

**LONDON,** England

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Ange Postecoglou, amesema kichapo cha mabao 3-2 cha timu yake kutoka kwa Brighton kwenye Ligi Kuu England ni kibaya zaidi tangu ajiunge na timu hiyo.

Tottenham walimaliza kipindi cha kwanza wakiwa mbele kwa mabao 2-0 baada ya mabao ya Brennan Johnson na James Maddison kabla ya kufungwa mara tatu katika kipindi cha pili.

"Ilikuwa ya kukatisha tamaa na nimechoshwa na hilo," alisema Postecoglou.

"Ni kipindi cha pili kisichokubalika - hatukuwa karibu na tulipopaswa kuwa. Labda tulibebwa na jinsi tulivyokuwa tukienda.

"Tulikubali hatima yetu na ni ngumu kuelewa kwani hatujafanya hivyo nikiwa hapa. Kawaida tunapigania kila kitu."

Tottenham wangeingia kwenye nne bora kama wangeshinda mchezo huo na Brighton wako nafasi ya sita kwenye msimamo.

Postecoglou alikosoa tabia ya timu yake ya kuridhika katika kipindi cha pili, na kuongeza: "Labda mambo yalikuwa yanakwenda vizuri sana. Soka na maisha vitakukwaza ikiwa utatangulia mbele yako na ndivyo ilivyokuwa katika kipindi cha pili.

"Ni hasara mbaya kwetu, mbaya kama inavyozidi, na kuna njia moja tu ya kuirekebisha na hilo ni jukumu langu."

# Flick akunwa na fowadi Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Hansi Flick, ameisifu safu yake ya ushambuliaji chini ya Robert Lewandowski, Raphinha na Lamine Yamal, baada ya vinara hao wa LaLiga kushinda mabao 3-0 dhidi ya Alaves Jumapili.

Lewandowski alifunga mabao matatu 'hat-trick' kipindi cha kwanza huku Raphinha akitoa 'asisti' mbili na Barca ikarejesha kileleni wakiongoza kwa pointi tatu dhidi ya Real Madrid.

Hakuna mchezaji ambaye amehusika katika mabao mengi katika ligi tano bora za Ulaya msimu huu zaidi ya Lewandowski (mabao 10, asisti mbili), huku Raphinha (mabao matano, asisti nne) na Yamal (mabao manne, asisti tano).

"Kwa kweli tunashughulikia umoja wao," alisema Flick katika mkutano na waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Kila mazoezi na unapokuwa na mikutano, unawaonesha kutoka upande wa mbinu na pia nafasi ni muhimu sana. Wanafanya vizuri.

"Mwishowe, tunafunga mabao mengi ambayo ni mazuri kwetu na inatusaidia pia kwa mechi zinazofuata kuwa na imani hii katika mchezo wetu, katika wazo letu la kucheza mpira."

Katika mechi 11 kwenye mashindano yote, Barca sasa wameshinda kwa mabao matatu.

Katika mashindano yote, Lewandowski mchezaji wa Kimataifa wa Poland, sasa amefunga mara 12 na ana wastani wa zaidi ya bao kwa kila mchezo.

"Kila mtu anamuunga mkono Lewy na anajua la kufanya ndani ya kisanduku - mbele ya goli yeye ndiye mchezaji bora kwangu," aliongeza Flick.

"Amekuwa wa kustaajabisha kwa kipindi hiki, kufunga hata mabao, ni vizuri sana. Nina furaha naye sana. Unaweza kuona yuko fiti kwa asilimia 100 na wachezaji wenzake wanamuunga mkono vizuri."

Raphinha, ambaye alikuwa nahodha wa Barca dhidi ya Alaves, pia amekuwa katika kiwango kizuri msimu huu. Mkwaju wake wa faulo ulitengeneza bao la kwanza la Lewandowski dhidi ya Alaves na akaongoza shambulizi la kaunta ambalo liliisha na la pili pia.

Barca sasa wameshinda mechi nane kati ya tisa za mwanzo za LaLiga chini ya Flick, sita kati yake wakiwa ugenini, na kufunga mabao 28.

## Simba, Yanga mtegoni CAF

INATOKA UK. 24

ndani kwenye Kombe la Shirikisho, lakini mwaka huu wameboresha kikosi chao, Al Hilal nao pia tumeshawahi kukutana nao, ni timu ambayo imeendelea kulinda kiwango chao, iko vile vile, haijaporomoka kiwango pamoja na kwamba nchini kwao kuna matatizo ya vita na hawana ligi nyumbani, si timu ya kubeza ni timu iliyojipanga tuliona ilipokuja kucheza hapa na Algeria tumeshakwenda mara kadhaa tunazifahamu timu za huko," alisema Arafat.

Pamoja na hayo alisema wao wanajipanga kuipeperusha vizuri bendera ya Tanzania akiwataka mashabiki kujazana kwa wingi viwanjani wakati timu hiyo ikicheza.

"Uzuri ni kwamba sisi kama Yanga tuna kikosi kizuri, bora na tumejipanga kuhakikisha timu yetu inafanya vizuri msimu huu, wachezaji wetu walikuwa hapa, wameona jinsi viongozi wao na mashabiki wao walivyokuwa na hamasa wakati wa upangaji wa droo," alisema.

Ofisa Habari wa Simba, Ahmed Ally, alisema wamefurahi kucheza na timu ambazo hawajawahi hata siku moja kukutana nazo kwenye michuano ya Afrika.

"Tumefurahi aina ya wapinzani ambao tumepangiwa, kwanza kwetu ni wapinzani wapya hatujawahi kukutana kwenye pilikapilika zetu kwenye michuano ya makombe ya Afrika, tutakwenda kucheza Algeria, tutakwenda kucheza Tunisia nchi ambayo kwa miaka ya karibuni hatujawahi kwenda kucheza mechi yoyote ile, kwa hiyo msimu huu tunakwenda kucheza tukiwa na wapinzani wapya kabisa.

"Angola tuliwahi kwenda kucheza na Primeiro de Agosto, Algeria tulikwenda kucheza na Mo Bejaia," alisema Ahmed ambaye amesema wamejiandaa kukabiliana na timu hizo.

Timu za Tanzania zote zitaanzia nyumbani, Yanga ikianza Novemba 26 au 27 dhidi ya Al Hilal Ligi ya Mabingwa, Simba ikikipiga Novemba 28 dhidi ya Bravo do Maquis.

Pia zitamalizia mechi zao nyumbani, Yanga ikicheza dhidi ya MC Alger, Januari 17 au 18, kabla ya Simba kushuka Januari 19, mwakani dhidi ya CS Costantine ya Algeria.

# WACHEZAJI SIMBA WAPEWA ANGALIZO USAJILI DIRISHA DOGO

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Simba imesema itafanya usajili wa wachezaji wapya kipindi cha dirisha dogo la usajili na kuondoa wale ambao watashindwa kuonesha ubora wao mpaka kufikia Desemba na Januari mwakani.

Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Klabu hiyo, Salim Abdallah 'Try Again', amesema kuwa kwa sasa wana malengo makubwa ya kufanya vizuri kwenye michuano ya ndani na nje ya nchi huku ikiwa imefanya mabadiliko makubwa kwenye kikosi, hivyo wanategemea wachezaji waliopo kuonesha ubora na kuipambania klabu na si vinginevyo.

"Ni kweli, tutaboresha tena kikosi chetu kipindi cha dirisha dogo, tunaangalia wachezaji ambao wamefanya vizuri na wapo kwenye ubora na wapambanaji kuipigania nembo ya klabu tutabaki nao, wale ambao wameshindwa kuonesha ubora wao kwa namna moja ama nyingine au kwa sababu mbalimbali, tutawapunguza ili kuleta wengine ambao wanaweza kuleta upinzani katika kikosi chetu," alisema Try Again.

Mjumbe huyo ambaye ni Mwenyekiti wa zamani wa Bodi ya Wakurugenzi, alisema wanataka kuifanya Simba kuwa klabu tishio si Tanzania tu, bali Afrika nzima, hivyo watasaka mchezaji yeyote mzuri ambaye anafaa kuicheza klabu yao na kumleta kwenye kikosi chao.

**"Jambo kubwa ni kuhakikisha Simba inarejea katika ubora wake, mimi nilipomwachia kijiti Mohamed Dewji, tulikubaliana kwamba lazima Simba irudi kwenye ubora wake na kwa mbali mmeanza kuona mabadiliko.**

"Tumefanya mabadiliko makubwa kwenye kikosi chetu, tumesajili vijana wengi wadogo ambao wanahitaji muda kuweza kuendana na mazingira ya mpira wetu.

"Unaweza kuona wachezaji wengi tuliowaleta wa kikosi cha kwanza, pia tumesajili vijana wa ndani ili kujifunza kutoka kwa hawa tuliowaleta," alisema.

Baada ya kumalizika kwa Ligi Kuu msimu uliopita, klabu hiyo iliondoa wachezaji wake wengi waliokuwa tegemeo kwenye kikosi hicho kwa muda mrefu, akiwamo nahodha, John Bocco, Clatous Chama, Saido Ntibazonkiza, Sadio Kanoute, Kennedy Juma na wengine wengi, huku ikisajili wachezaji 14 wa ndani na nje ya nchi ambao tayari wameiwezesha timu hiyo kutinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika na tayari imeshacheza mechi tano za ligi, ikishinda nne na sare moja.

**TUTAWAMALIZA...**




Mashabiki wa timu ya Simba, waliokusanyika katika Tawi la Simba Asili lililoko Kawe, Dar es Salaam, kufuatilia droo ya hatua ya makundi Kombe la Shirikisho Afrika iliyokuwa ikipangwa jana jijini Cairo Misri, ambapo timu yao ilipangwa Kundi A sambamba , CS Sfaxien ya Tunisia, CS Constantine (Algeria) na FC Bravos do Maquis ya Angola. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## *Yanga yapewa onyo Ligi Kuu*

**Na Adam Fungamwango**

KAMATI ya Uendeshaji na Usimamizi ya Ligi, ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB), imeipiga faini Klabu ya Coastal Union na kuionya Yanga kwa makosa ya kuchelewa kufika uwanjani.

Taarifa iliyotolewa jana na TPLB, imesema Klabu ya Yanga imepewa onyo kali kwa kosa la kuchelewa kufika kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, kuelekea mchezo wao wa Ligi Kuu dhidi ya KMC ambao uliisha kwa wao kupata ushindi wa bao 1-0, Septemba 29, mwaka huu.

Katika taarifa hiyo ya TPLB imeeleza kuwa Yanga ilifika uwanjani saa 1:48 usiku, badala ya saa 1:30 usiku na hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 17:15 ya Ligi Kuu kuhusu taratibu za mchezo.

Imeeleza adhabu hiyo imetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 17:62 ya Ligi Kuu kuhusu taratibu za mchezo.

Klabu ya Coastal Union, imetozwa faini ya Sh. milioni moja, kwa kosa la kuchelewa kuiwasilisha orodha ya wachezaji na maofisa wa ufundi kuelekea kwenye mchezo wao dhidi ya Mashujaa FC, uliochezwa, Septemba 13, mwaka huu, Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, kinyume cha matakwa ya Kanuni ya 17:6, huku adhabu ikitolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 17:62, mchezo huo ambao ilifungwa bao 1-0.

Coastal, pia imepewa onyo kwa kosa la kuchelewa kuwasilisha listi ya wachezaji, benchi la ufundi na viongozi wake kuelekea kwenye mchezo wa Ligi Kuu kati ya timu hiyo dhidi ya KMC, Agosti 29, mchezo uliomalizika kwa sare ya bao 1-1, mechi ilipigwa, KMC Complex, Mwenge.

Taarifa ilieleza timu hiyo iliwasilisha orodha yake saa 7:50 mchana, badala ya saa 7:00 mchana kama ilivyoainisha kwenye Kanuni ya 17:6, adhabu ikitolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 17:62.

# Michezo

Jumanne Oktoba 8, 2024
Nipashe



Flick akunwa na fowadi Barca UKURASA 22




# Simba, Yanga mtegoni CAF

## ●●● Wekundu wa Msimbazi katika kundi la kifo, lakini wasema robo fainali inawahusu, Wananchi watamba...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Mabingwa wa Tanzania Bara wakipangwa Kundi A kwenye hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika ikiwa na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Al Hilal ya Sudan na MC Alger ya Algeria, wawakilishi wa nchi kwenye Kombe la Shirikisho, Simba nao wamepangwa Kundi A, likitajwa kuwa ni kundi la kifo.

**Simba inatarajiwa kuanzia nyumbani dhidi ya Bravo do Maquis ya Angola, Novemba 28, kama ilivyo kwa Yanga ambayo nayo itaikaribisha Al Hilal kati ya Novemba 26-27, mwaka huu.**

Makamu Rais wa Klabu ya Yanga, Haji Arafat, amesema hakuna timu rahisi katika kundi lao, bali ubora wa vikosi ndivyo vitakavyoamua, huku lengo lao likiwa ni kivuka hatua ambayo waliishia msimu uliopita.

Kwa mujibu wa droo iliyopangwa jana Makao Makuu ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), jijini Cairo, Misri, Simba iko kundi moja na timu za CS Costantine ya Algeria, na CS Sfaxien ya Tunisia.

CAF, imelitaja kundi hilo kuwa la kifo kutokana na ubora wa timu zilizoko, ikiwamo Simba yenyewe ambayo imekuwa ikifanya vema kwenye michuano ya kimataifa.

Klabu ya CS Sfaxien, ambayo imelitwaa Kombe la Shirikisho Afrika mara tatu, 2007, 2008 na 2013, ikiwahi pia kulitwaa 1998 wakati likiitwa Kombe la CAF, ambapo Simba ilifika fainali 1993.

Timu hiyo ilifika fainali ya Kombe la Shirikisho 2010, lakini pia ilicheza fainali tatu za Super Cup, inayochezwa dhidi ya Mabingwa wa Afrika na Kombe la Shirikisho, 2007, 2009 na 2014 na kupoteza.

CS Sfaxien ilifika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika mwaka 1996 na 2006, huku ikifika fainali 2014. Yanga itakutana tena na timu tatu ambazo imeshawahi kukutana nazo kwenye hekaheka za michuano hiyo.

Itacheza na MC Alger ambayo ilikutana nayo kwenye hatua ya makundi, Kombe la Shirikisho, Aprili 8, 2017, ikishinda bao 1-0 nchini na kwenda kupoteza kwa mabao 4-0 ugenini, Aprili 15, 2017.

Kwa mara nyingine tena itavaana uso kwa uso na TP Mazembe ambayo msimu 2022/23, ilikutana nayo kwenye hatua ya makundi Kombe la Shirikisho, ikishinda mabao 3-1, Februari 19, 2023 nchini na kwenda kushinda tena ugenini nchini DR Congo bao 1-0.

Kwenye kundi hilo pia kuna Al Hilal ambayo iliinyima Yanga nafasi ya kwenda hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika 2022/23, na badala yake kuangukia Kombe la Shirikisho.

Katika mchezo wa raundi ya kwanza, timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1, Oktoba 8, 2022, mchezo ukipigwa hapa nchini, na Yanga kuchapwa bao 1-0 katika mchezo wa marudiano nchini Sudan, uliochezwa Oktoba 16, 2022.

Hata hivyo, kwa mujibu wa CAF, kwenye Ligi ya Mabingwa, Mabingwa Watetezi, Al Ahly, iliyopo Kundi C sambamba na CR Belouizdad ya Algeria, Orlando Pirates (Afrika Kusini) na Stade d'Abidjan ya Ivory Coast, ndilo linaloelezwa kuwa gumu zaidi.

"Hatua hii hakuna timu rahisi, timu zote ambazo zimeingia kwenye hatua hii ni ngumu na zina malengo ya kufika mbali, TP Mazembe tuliwafunga nje na

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >